Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 1 Februari, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko napenda kuliarifu rasmi Bunge kwamba aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Mheshimiwa Frank Michael Mussati, alifariki dunia tarehe 14 Novemba, 2004 katika ajali ya basi alilokuwa anasafiria akitokea Dar es Salaam kwenda Morogoro. Kwa utaratibu wetu wa kawaida naomba sasa tusimame kwa dakika moja kumwomba Mwenyezi Mungu aweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kumkumbuka Mheshimiwa Frank Michael Mussati aliyekufa katika ajali ya gari)*

**SPIKA:** Naomba kutoa taarifa zaidi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Rais alimteua na kumwapisha Katibu mpya wa Bunge, ambaye sasa napenda kumtambulisha kwenu Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Damian Foka, atasimama tumwone wote vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo ni taarifa ya Miswada tuliyoipitisha katika Mkutano wetu wa mwezi Novemba, 2004. Mtakumbuka kwamba jumla ya Miswada sita ilipitishwa na Bunge hili, katika hiyo sita, mitatu ilishamalizwa kuchapishwa upya pamoja na marekebisho yaliyofanywa na Bunge na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais na imeshapata kibali chake. Mitatu mingine bado haijachapishwa kwa sababu Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali amekuwa na kazi nyingi hapa karibuni, hakuweza kukamilisha uchapaji wa Miswada yote sita.

Kwa hiyo, Miswada mitatu imeshakuwa Sheria, mitatu bado inasubiri kufikishwa kwa Mheshimiwa Rais.

Mwisho wa matangazo. Tunaendelea na *Order Paper.*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Ujenzi wa Ukumbi wa Bunge

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa Ukumbi wa Bunge Dodoma umeanza rasmi:-

(a) Je, ni kampuni gani imepewa *tender* ya ujenzi huo?

(b) Je, ujenzi utagharimu kiasi gani cha fedha hadi kukamilika?

(c) Je, ujenzi huo utachukua muda gani hadi kukamilika na kukabidhi kazi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuhura Shamis Abdallah, Mbunge wa Kiwani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kampuni iliyoshinda *tender* ya ujenzi wa Ukumbi mpya wa Bunge ni *China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC)* kwa kushirikiana na Kampuni ya *China Railway Jianchang Engineering (CRJE).*

(b) Mheshimiwa Spika, gharama ya ujenzi *(construction)* ya Ukumbi mpya baada ya uhakiki ni shilingi 24,860,224,257/60.

(c) Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi ilianza rasmi tarehe 1 Oktoba, 2004 ambapo mkandarasi alikabidhiwa eneo la kiwanja na inatakiwa kukamilika katika kipindi cha majuma 52 ambayo yanaishia tarehe 28 Novemba, 2005, tarehe ambayo makabidhiano rasmi yatafanywa kati ya wawekezaji na Serikali na tarehe 10 Februari, 2005 jiwe rasmi la msingi litawekwa.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kazi ya ujenzi wa Ukumbi wa Bunge itakamilika kama ilivyopangwa.

**MHE. ZUHURA SHAMIS ABDALLAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Waziri, naomba kumwuliza swali moja dogo la nyongeza. Ukilinganisha sifa za kumbi za Bunge katika Afrika, je, sisi tunaweza kuwa na sifa katika kiwango gani? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Spika, imefanya utafiti kwanza kabla ya kuingia mkataba wa ujenzi na mchoraji, imefanya utafiti katika mabunge mbalimbali. Nataka kuwahakikishieni kwamba ramani iliyoteuliwa ambayo mlionyeshwa Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuanza ujenzi, ni miongoni mwa ramani na michoro ambayo italiwezesha Bunge letu kuwa katika kiwango cha Kimataifa.

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali la nyongeza, kwa vile maeneo muhimu katika jengo la Bunge ni maeneo ambapo raia watakuja kukaa na kusikiliza majadiliano ya Bunge inaitwa *Gallery* na kwa vile jengo la Chimwaga hapo awali lilitarajiwa ndiyo Makao Makuu ya Bunge la Tanzania na hatukuweza kufanya iwe hivyo, kwa sababu ya kutokuwa na *Gallery.* Je, jengo jipya la Bunge litakuwa na *Gallery* yenye hadhi na sifa inayotakiwa?

**MBUNGE FULANI:** Ole.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nitoe maelezo ya nyongeza kwamba jengo hili mpaka sasa siyo mali ya Serikali, jengo hili linajengwa na wawekezaji, mashirika ya Hifadhi ya Jamii kwa umoja wao ndiyo wanaowekeza hapa, wakishamaliza Bunge litatumia ukumbi huo kwa mkataba ambao wamefanya na Wizara ya Fedha kama wapangaji mpaka hapo tutakapomaliza deni kwa utaratibu huo wa kupanga na hivyo tutakabidhiwa jengo letu.

Kwa hiyo, mpaka sasa si jengo la Serikali. Lakini nataka kumhakikishia Mheshimiwa Phillip Marmo kwamba yale yote anayoyaona katika ukumbi huu, yemeboreshwa katika ukumbi mpya. Yapo maeneo mengi yamewekwa katika jengo hilo jipya. Lakini pia iko hatua ya pili itakayoendelezwa baada ya kumaliza hiyo *tender* ya kujenga maeneo mengine ambayo yamebakizwa katika ramani, kama *Car Park* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, namshauri tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu michoro hii tunayo, mwenye nafasi anaweza kurejea tena iko pale Ofisi ya Spika, mnaweza mkajiridhisha, mkajua ni huduma gani muhimu zilizopo katika hiyo *tender* ikiwa ni pamoja na hiyo *Gallery.*

Na. 2

**Ugawaji wa Wilaya na Majimbo**

**MHE. STEPHEN M. KAZI (k.n.y. MHE. RAPHAEL N. MLOLWA)** aliuliza:-

Kwa kuwa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002 yametoa takwimu zinazovutia sana ambapo zipo Wilaya na Majimbo yenye idadi ya watu wasiozidi 50,000 na Wilaya na Majimbo mengine yana watu zaidi kama Wilaya ya Kahama yenye watu 600,000 na Jimbo la Kahama watu 350,000 na kwa kuwa ugawaji wa Wilaya na Majimbo ni zoezi la Kikatiba ambalo hufanyika kila baada ya miaka 10:-

Je, Serikali ina mtazamo na mikakati gani katika kugawa zaidi maeneo ya utawala na uwakilishi wa nchi yetu kwa lengo la kurahisisha utawala, kusogeza huduma kwa wananchi na kuleta maendeleo sawia kwa Watanzania wote?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maudhui ya swali hili inafanana kabisa na maswali kadhaa yaliyojibiwa katika Bunge lako Tukufu kufuatia maswali mengine yaliyoulizwa kwa nyakati tofauti na Waheshimiwa Wabunge wafuatao:-

(i) Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake namba 2487;

(ii) Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, swali lake namba 1908;

(iii) Mheshimiwa Lucas Selelii, Mbunge wa Nzega, swali namba 1750;

(iv) Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, swali lake namba 1308;

(v) Mheshimiwa Khalid Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, swali lake namba 1101; na

(vi) Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, swali lake namba 3908. Kwa maana hiyo, dhana ya swali hili sio mpya, kwa hivyo nitaomba kulijibu kwa ufupi lakini kwa ufasaha zaidi ili kukidhi mahitaji ya Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya utawala yanayozungumziwa katika swali hili ni Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Tarafa na Kata ambayo yana uongozi au utawala wa Serikali. Wakati majimbo ni maeneo ya uwakilishi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 75 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Uchaguzi inayo mamlaka ya kugawanya Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi baada ya kupata kibali cha Rais na yaweza mara kwa mara na angalau kila baada ya miaka 10 kuchunguza mgawanyo wa majimbo. Kutokana na uchunguzi huo, Tume inaweza kubadilisha majimbo ya uchaguzi. Hata hivyo, Tume katika uchunguzi huo huzingatia vigezo vifuatavyo:-

(i) Idadi ya watu;

(ii) Hali ya kijiografia na uchumi wa eneo;

(iii) Jimbo la uchaguzi lisiwe ndani ya mipaka ya Wilaya mbili za kiutawala;

(iv) Jimbo lisiwe ndani ya mamlaka mbili tofauti za Serikali za Mitaa; na

(v) Jimbo liundwe na Kata ambazo Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amezitangaza kwa mujibu wa Sheria Na. 7 na 8 zote za mwaka 1982 na kuwa Kata hizo ni mahsusi kwa uchaguzi wa Madawani.

Mheshimiwa Spika, hivyo, idadi ya watu ni miongoni mwa vigezo muhimu na pekee hakitoshelezi kufanya majimbo ya uchaguzi yagawanywe. Tume itachunguza na kugawa majimbo ya uchaguzi yale tu ambayo yatakidhi vigezo hivyo vilivyotajwa kwa wakati muafaka.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Waziri.

Lakini imebainika wazi kwamba suala la majimbo namna ya kuyagawa bado ni tatizo kwa Wabunge wengi kutokana na ile hadhi kwamba limerudiwa rudiwa. Sasa swali ni kwamba kwa nini Wizara inakuwa nyuma katika kuleta mawazo haya ya kugawa majimbo mapema badala ya kusubiri Wabunge walalamike?

Pili, katika majimbo au maeneo ambayo sasa yamebainishwa kwamba yagawanywe kwa mfano katika kipindi hiki, ni lini Tume au Wizara itatangaza rasmi mgawanyiko huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kwanza sidhani kwamba Waheshimiwa Wabunge wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wao kuihoji Serikali kuwa ni jambo ambalo nafikiri wanataka kujua taarifa hiyo. Kwa hivyo Wabunge hawalalamiki bali ni wajibu wao, ninawapongeza sana Wabunge kwa maswali yao yote waliouliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba tumezungumza hapa kwamba viko vigezo maalum ambavyo vinafuatwa kwa ajili ya kuongeza majimbo na kama vigezo hivyo havikutimia haviwezi kutekelezwa. Lakini la msingi ni kwamba nadhani tusubiri wakati muafaka mpaka hapo Tume itakapoona kwamba kuna haja ya kufanya hivyo.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ilisikika mwaka jana ikisema kwamba haina mpango wa kugawa majimbo kwa sasa na kwa kuwa jimbo la Moshi Vijijini, Halmashauri yetu ina mpango wa kuligawa, je, tunayo haki ya kufanya hivyo, baada ya Tume kusema kwamba haina mpango kwa sasa? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MUHAMMED SEIF KHATIB):** Mheshimiwa Spika, mamlaka ya kugawa majimbo haifanywi na Halmashauri yako wala mtu mwingine, isipokuwa Tume inapendekeza na Rais anakubali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwenye mamlaka ya mwisho ya kutoa kibali ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Katiba yetu. Kwa hivyo na sisi Wabunge inafaa tufuate Katiba yetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa sasa hivi ninawashauri Waheshimiwa Wabunge kwamba muda uliobakia ni mdogo sana na hayo majimbo nafikiri ni makubwa kuna watu wananyemelea huko waliko. Kwa hiyo, ningeshauri ujiandae kuyalinda kusudi urejee hapa mwakani. *(Kicheko)*

Na. 3

**Kupunguza/Kuondoa Umaskini**

**MHE. KHALID S. SURU** aliuliza:-

Kwa kuwa suala la kuondoa/kupunguza umaskini ni pamoja na kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ambayo itaharakisha kuwawezesha wananchi kupata uwezo wa kupiga hatua kubwa ya kuondoa umaskini wa huduma na wa kipato; na kwa kuwa Wilaya ya Kondoa ni miongoni mwa Wilaya zilizopania kupunguza na hatimaye kuondoa umaskini kwa kiwango kikubwa kupitia miradi ya wananchi wenyewe, Serikali, wahisani na mashirika yasiyo ya Kiserikali:-

(a) Je, kuanzia mwaka 1996 hadi mwaka 2004, Serikali yenyewe pamoja na mashirika ya *IFAD, SNV, BSF, Water Aid,* Benki ya Dunia, *NAEP, HIPIC* na kadhalika, kwa pamoja walitekeleza/wametekeleza miradi au shughuli zilizogharimu fedha kiasi gani kwa dola za Kimarekani na kwa shilingi ya Tanzania?

(b) Je, miradi ya kilimo na ufugaji imechukua asilimia ngapi ya fedha zote zilizotajwa katika sehemu (a) ya swali hili?

(c) Kwa kuwa sasa hivi ajira ni hoja yenye kero sana miongoni mwa vijana wetu wa kike na kiume; je, Serikali ina mikakati gani ya sasa na ya baadaye ya kukabiliana na hali hiyo inayoongezeka kwa kasi kubwa hapa nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalid Suru, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya tatu inaendelea kutekeleza mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali ili kupunguza umaskini.

Kupitia Wizara mbalimbali Serikali katika kipindi cha mwaka 1995/1996 - 2003/04 ilitumia wastani wa shilingi 2,135,352,000,000 (Trilioni mbili bilioni 135 milioni 352) karibu sawa na dola za Kimarekani 2,135,352,000 (Billion 2 milioni 135 352) kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo hapa nchini. Fedha hizi zinajumuisha fedha za Serikali na Wafadhili. Taarifa hii imetokana na ripoti ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya mwaka 2003 *(Economic Survey 2008).* Kiasi cha fedha kilichotumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo kutoka katika Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Jumuia za Kiraia na wananchi wenyewe siyo rahisi kufahamika. Fedha hizi ni nje ya mipangilio ya fedha za Serikali na pia wengine huchangia vifaa, nguvu kazi ambavyo siyo rahisi sana kukusanya taarifa zake.

(b) Asilimia ya bajeti yote ya Serikali iliyoelekezwa katika sekta ya kilimo ni 5. Asilimia 55 ya fedha zote zilizoelekezwa katika sekta ya kilimo zilitumika kwenye miradi ya kilimo. Taarifa hii imetokana na uchambuzi wa takwimu zilizopo katika kitabu cha nne cha Makadirio ya Fedha za Serikali (sehemu A) Mipango ya Maendeleo ya Wizara na Mikoa kwa miaka ya 1995/1996 - 2004/2005.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali katika kukabiliana na tatizo la ajira kwa vijana hapa nchini ikiwemo Mpango wa kuendesha mafunzo juu ya utaratibu wa watu kuweza kujiajiri na kuondoa umaskini *(Demand-Driven Skills Training Programme).*

Aidha, Kituo cha ajira chini ya Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo huwasiliana na waajiri mbalimbali nchini na kufanikiwa kupata nafasi za kazi zipatazo 708 kwa mwaka wa fedha ulioisha. Jitihada zinaendelea kutafuta nafasi za ajira kwa vijana wengi zaidi. Katika kuboresha huduma, Kituo cha ajira kilifanya utafiti kuhusu uridhishaji wa waajiri *(Employers Satisfaction Survey)* katika Mkoa wa Dar es Salaam na kugundua kwamba kati ya waajiri waliowahi kutumia huduma za kituo hicho asilimia 89 wanaridhika na huduma za Kituo hiki kwa kiwango kikubwa. Pia warsha mbalimbali za mafunzo hutolewa ili vijana waweze kujitafutia ajira.

Aidha, Serikali chini ya Ofisi ya Rais imeandaa Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za wanyonge Tanzania *(MKURABITA)* ili waweze kutoka kwenye sekta isiyo rasmi kwenda kwenye sekta rasmi. Mpango huu utaongeza idadi ya ajira kwa namna mbalimbali. Kwa mfano, uwezo wa kukopa toka kwenye taasisi za mikopo utaongezeka na hivyo wananchi kupata mitaji.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa mipango ya baadaye ya kuboresha ajira, mikakati ya makusudi imebainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini *(MKUKUTA)* ambao unatarajiwa kupitishwa na Serikali hivi karibuni. Mikakati hii ilibainishwa na vijana wenyewe wakati wa mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini wa awali *(PRS)* iliingizwa katika *MKUKUTA* na imejumuisha mambo yafuatao:-

Uelimishaji wa vijana katika fani mbalimbali za kazi, kutoa nafasi zaidi katika vyuo vya juu, kuwezesha upatikanaji wa mikopo na kuelimishana kuhusu miradi mbalimbali ya maendeleo, kuendelea kuboresha juhudi zilizokwisha anzishwa na Serikali na kadhalika.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa majibu mazuri katika swali langu la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umaskini unaweza kuondoshwa kwa kiwango kikubwa na vijana wetu wa kike na wa kiume ambao ndiyo nguvu kazi kabisa ya Taifa letu. Lakini vikwazo vikubwa ni kukosa zana za kisasa za kuzalisha mali kama matrekta madogo, jembe la kukokotwa na wanyama, maeneo ya kulima na uhakika wa mitaji. Je, kwa kuwa kule Kondoa vijana wapo tayari kabisa katika shughuli hizi za kilimo Ofisi ya Makamu wa Rais itawasaidiaje hao vijana ili waweze kuondoa umaskini kwa njia hiyo? *(Makofi)*

Pili, kwa vile vijiji vyote na mitaa yote nchini haina wataalam waajiriwa ambao wanaweza kabisa wakapanga mipango ya kuendeleza vijiji na mitaa, je, Serikali kwa nini isianzishe ajira ya wataalam hao wakaenda huko vijijini kwa nia ya kupata ajira ya vijana na kwa nia vile vile ya kuondoa umaskini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba nguvu kazi kubwa ipo mikononi mwa vijana wetu wa kike na wa kiume na ndiyo maana katika suala zima la kuondoa umaskini kilimo hicho anachokisemea ni sehemu mojawapo ya mkakati wa kuondoa umaskini unaoishia sasa au sekta mojawapo ambayo imepewa kipaumbele na ni kazi yetu sisi wote kwa ujumla kwa maana ya Serikali hususan Wizara ya Kilimo na Chakula kuhakikisha kwamba mipango ambayo inawekwa inazingatia utumiaji wa nguvu kazi katika kila Mkoa kutegemeana na mazao ambayo yanaweza kuondoa umaskini

yakielekezwa kwa mfano mikoa ya Kusini zao la korosho, ukielekeza vijana nguvu kazi yao ielekee kwenye korosho. *(Makofi)*

Upande wa ziwa kwa mfano, kuboresha na kuimarisha kilimo cha pamba ili kiwe kina lengo hilo hilo la kuondoa umaskini pamoja na uvuvi na kadhalika na kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba Waziri mwenzangu Mheshimiwa Charles Keenja, yuko hapa na kwa vyovyote vile anayo mipango ambayo inazingatia mwelekeo huo na kama nilivyosema kwenye mpango mpya ambao tunatazamia wiki hii upitishwe na Serikali tutakuwa tumezingatia zaidi kulenga kuondoa umaskini ambao unapambana zaidi na umaskini wa kipato ndiyo unaokera zaidi.

Kuhusu mafunzo ya wataalam, bila shaka Mheshimiwa Khalid Suru, anaelewa kwamba kupitia Wizara ya TAMISEMI na Halmashauri za Wilaya yametolewa maelekezo mbalimbali ya kuhakikisha kwamba Halmashauri zetu zinaweka utaratibu ambao unatambua uwezo wa vijana katika kila eneo ili kuweza kuelekeza namna vijana wetu wanavyoweza kutumia nguvu kazi yao kwa kujiajiri wenyewe na hata kuajiriwa katika maeneo ambayo yanapatikana ajira hizi za kawaida. Kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na Serikali za Mitaa hasa katika kuhakikisha tunatekeleza sera hizi za kuondoa umaskini.

Na. 4

**Kutajwa Zanzibar kama Mkoa**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005 ukurasa wa 107 Zanzibar imeingizwa katika orodha ya Mikoa kama ilivyo kwa Mikoa ya Mtwara, Singida, Lindi na kadhalika; na kwa kuwa hata katika sehemu ya Wilaya, iliandikwa Wilaya ya Unguja na Pemba; na kwa kuwa Zanzibar ni nchi yenye Mikoa mitano na Wilaya kumi:-

(a) Je, kuiweka Zanzibar katika orodha ya Mikoa kuna tafsiri gani?

(b) Je, kuainisha kuwa Zanzibar ina Wilaya ya Pemba na Unguja kuna tafsiri gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubali kwamba kwenye jedwali ukurasa wa 107 wa kitabu cha hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Julai, 2004) inaonekana taarifa inaamsha hisia potofu ya tafsiri kuwa Zanzibar ni Mkoa na ina Wilaya za Unguja na Pemba. Hatukuwa na maana

hiyo kwani inafahamika popote pale kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye Mikoa mitano na Wilaya kumi na hakuna shaka lolote kuhusu hilo na halina mjadala.

Mheshimiwa Spika, tafsiri iliyotumika katika vipengele vyote viwili, kwa upande wa Zanzibar ni ya kiutendaji/utekelezaji ili kuhakikisha huduma ya Mifuko ya *TASAF* na *SELF* inafika Zanzibar na kuleta manufaa makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo haya, marekebisho yatafanyika kwenye jedwali hilo ni maeneo ya miradi yote kwa sehemu zote mbili za nchi yasomeke kama yanavyoeleweka kiutawala. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajitahidi kadri ya uwezo wake kuleta maendeleo kwa nchi zake zote mbili yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Shughuli nyingi za maendeleo hufanyika pande zote kulingana na uwezo wa Serikali, kwa mfano, kila mwaka asilimia 4.5 ya misaada inayotolewa na wahisani, Serikali huelekezwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, aidha, moja ya mikakati na mipango ya Serikali katika kupambana na umaskini ni kuwawezesha na kuunga mkono jitihada za wananchi ili kupambana na umaskini wa kipato na ule usio wa kipato. Hivyo basi Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* imeanzisha mradi wa *SELF* ambao unatoa mikopo yenye gharama nafuu kwa Asasi za fedha, zikiwemo *SACCOS,* ili nao watoe mikopo kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ambao umekuwa ukiunga mkono nguvu za wananchi katika kuimarisha miundombinu katika maeneo ya barabara, elimu, afya, maji na kadhalika. Mradi wa *SELF* sasa umepanua eneo la mradi kufikia mikoa 14 Tanzania Bara na utatekelezwa mikoa yote ya Zanzibar (Unguja na Pemba). *TASAF* kuanzia mwezi Januari 2005 itatoa huduma nchi nzima, yaani Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa huduma hizi una masharti yake. Mifuko yote hii miwili inatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ilihusisha Mikoa na Wilaya chache kwa upande wa Tanzania Bara na ilihusisha Zanzibar nzima yaani Unguja na Pemba. Vigezo vya kiasi gani cha fedha kitolewe sehemu fulani zinazingatia, pamoja na mambo mengine, sababu za kijiografia, ukubwa wa eneo, idadi ya watu na hali ya umaskini. Eneo ambalo ni kubwa lina idadi kubwa ya wakazi na lina umaskini uliokithiri linapatiwa fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo wakati upande wa Tanzania Bara mipaka ya kiutawala (Mikoa, Wilaya) imefuatwa kubainisha maeneo ya kiutekelezaji na kwa upande wa Zanzibar mgawanyo umefanywa kwa kuzingatia eneo la utekelezaji *(Operational area)* kwa kuchukua Zanzibar kama eneo moja la utekelezaji lenye sehemu mbili yaani Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya ujumla yamekuwa marefu kutokana na unyeti wenyewe wa suala hili. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya maelezo hayo ningependa kujibu sehemu (a) na (b) ya swali hilo kama ifuatayo kwa kifupi tu. *(Makofi/Kicheko)*

(a) Jedwali namba moja la mgao wa fedha za mradi wa *SELF* linaonyesha mgao huo kwa mikoa na Wilaya kwa Tanzania Bara na Zanzibar (Unguja na Pemba) mgao umeonyeshwa kwa kufuata *operational area* siyo kwa tafsiri ya kiutawala, kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya utangulizi.

(b) Jedwali namba mbili linaonyesha mgao wa fedha za *TASAF* kwa Wilaya zote (kiutawala) zilizonufaika kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar kama *operational area* kwa sehemu zake mbili za utekelezaji yaani Unguja na Pemba kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya utangulizi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwamba amekiri yale ambayo yana ukosefu. Lakini hata hivyo napenda kuuliza maswali ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa kumbukumbu zinavyoandikwa na ndivyo zinavyosemeka. Je, zilizokuwa wamekwishaandika na vitabu ni moja katika kuweka historia, vipi wataweza kuvifuta vitabu hivyo na kuainisha kama inavyostahili dhidi ya Zanzibar?

La pili, kwa kuwa imeonyesha kwamba mgawanyo wa mapato unakuja kwa Zanzibar na kwa kuwa Zanzibar ina Mikoa yake na Wilaya zake haoni kwamba Zanzibar inadhulumika katika mgawanyo huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kuhusu kwamba hili limekwisha andikwa tayari kwenye vitabu vya kumbukumbu, natumaini ana maana ya *Hansard.* Hili wala lisimtie wasiwasi, kwa sababu Bunge ni kitu kinachoendelea, vikao vyake kama sisi tumefafanua wala hatukusema kwamba tulikosea isipokuwa tumefafanua tulikuwa na maana gani. Kwa hiyo, mtu yeyote anayefanya kwa mfano, utafiti au kujikumbusha akisoma ya Julai bila shaka atasoma na haya ninayoyasema sasa hivi kwa sababu haya nayo yanaandikwa. Kwa hiyo, kama yameandikwa yule atakuja kuona kwamba kumbe siku ile walifanya hivi wakasahihisha hapa. Kwa hiyo, mambo ya kumbukumbu wala yasimtie wasiwasi na nakupongeza Mheshimiwa Spika, kwa kudumisha utaratibu huu. Vinginevyo ingebidi tukasahihishe vitabu hivi lakini hamna sababu ya kufanya hivyo. *(Kicheko)*

La pili, kuhusu kwamba mgao Zanzibar inapunjwa, mimi sikubaliani naye kwa sababu limefanyika hivyo kwa kutazama ukubwa wa nchi yetu. Kwa maana Tanzania Bara, imeunganishwa na Zanzibar ukitazama sasa uwiano wa ukubwa wa maeneo ndio

tukapata hiyo 4.5%. Yenyewe hiyo ndio *static* yaani siyo kwamba ndio kama msahafu fulani ndio maana kuna ile Tume ya pamoja ya Mheshimiwa William Shellukindo ambayo tutafanyiwa semina kikao hiki hiki kutuelimisha zaidi maana yake ni kwamba kama kuna tatizo linatazamwa pale halafu mambo yanarekebishwa. Lakini kwa sasa uwiano huo hauna ubaguzi wala haumuonei mtu yeyote. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutoa maelezo juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri, kwa mujibu wa Katiba yetu Zanzibar ni nchi yenye Mikoa Mitano inajumlishwa inakuwa 26 ya Tanzania.

Je, kulikuwa na kosa gani kama inachukuliwa Zanzibar ni eneo la *operation area* ikatamkwa kwamba kwa sababu ya *TASAF* na ikaonekana pengine Mkoa wa Kusini Pemba lakini ikaonekana Zanzibar. Kwa nini ifanywe Zanzibar kama Mkoa? Hivi hatuoni kwamba inaidhalilisha Zanzibar kwa nini tusiende moja kwa moja kwamba ni Mkoa wa Kusini Unguja uliyoko Zanzibar?

**SPIKA:** Lakini Waziri amesema marekebisho yatafanyika kwenye jedwali hilo. Nadhani hukusikia majibu ya Waziri limeshajibiwa hilo. *(Makofi)*

Na. 5

**Uuzaji Holela wa Miwani ya Macho**

**MHE. ASHA A. NGEDE:** aliuliza:-

Kwa kuwa siku za hivi karibuni imejitokeza biashara ya kuuza miwani inayotumiwa na watu wenye matatizo ya macho inayofanywa na wafanyabiashara wadogo wadogo wa mikononi maarufu kama Wamachinga na kwa kuwa miwani hiyo haina vipimo maalum vya daktari wa macho, hivyo wananchi kwa kutojua madhara yake wanainunua miwani hiyo.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Je, huo uuzaji holela wa miwani hiyo una madhara gani?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya biashara hiyo barabarani?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Ngede, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inalifahamu tatizo la uuzaji holela wa miwani inayotumika na watu kwa ajili ya kujipamba zaidi kuliko ya matatizo ya macho kupitia kwa wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Wamachinga. Kwa wale wanaonunua miwani holela kwa sababu ya shida ya kuona kwa hakika ni kinyume kabisa na misingi ya utoaji huduma za tiba kwa jamii. Ni muhimu ieleweke ya kwamba miwani ni matibabu kama dawa nyingine ambazo ni lazima zitolewe kwa ushauri wa daktari baada ya vipimo maalum.

(b) Mheshimiwa Spika, uuzaji huu wa miwani barabarani una madhara makubwa kwa kuwa watumiaji wengi wa miwani hiyo, watakuwa wanatumia miwani ambayo si ya vipimo vyao hata kama ni urembo na kwa hiyo itawasababishia kupungua kwa upeo wao wa kuona mapema. Hivyo kusababisha ulemavu unaopunguza nguvu kazi ya Taifa.

(c) Mheshimiwa Spika, maoni ya Serikali juu ya biashara hiyo ya miwani kama ilivyo kwa dawa yoyote, kuuzwa barabarani ni batili na inapaswa kudhibitiwa kikamilifu kwa jinsi ambavyo uuzaji wa madawa mengine ya binadamu unavyodhibitiwa.

Sheria iliyopo hivi sasa ya udhibiti wa biashara ya miwani iko kimya kuhusu hatua zipi za kisheria zichukuliwe ili kudhibiti utoaji holela wa huduma hii. Wizara yangu inaandaa Muswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria hii ili iondoe mapungufu ya Sheria ya Awali ya mwaka 1966. *(Makofi)*

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri majibu yake ni mazuri na amelieleza Bunge hili kwamba biashara ya miwani ni moja ya biashara hatari, je, anaweza akatoa tamko la kupiga marufuku mara moja biashara hii hapa Bungeni?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nimekwisha kusema kwamba hii ni biashara batili. Lakini hata ukipiga marufuku kama sheria iko kimya, kwa yule anayeivunja inakuwa ni ngumu sana kuchukua hatua. Kwa hiyo, tunataka kwanza turekebishe na ni jambo dogo tu. Turekebishe kasoro hii kabla ya jambo hili halijachukuliwa hatua anayependekeza.

Na. 6

***Medical Store Department (MSD)***

**MHE. JOB Y. NDUGAI** aliuliza:-

Kwa kuwa *Medical Stores Department, (MSD)* ndiyo tegemeo kubwa kwa madawa na vifaa kwa hospitali zote za Serikali ikiwa ni pamoja na Vituo vya Afya na Zahanati; na kwa kuwa miaka ya hivi karibuni Idara hiyo imekuwa haina vifaa na madawa mengi muhimu ya kuuza;

Je, kwa nini Serikali inaendelea kulazimisha hospitali kununua dawa na vifaa kutoka *MSD* hata yale ambayo hayapatikani huko?

**WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Idara ya Bohari ya Dawa yaani *Medical Stores Department (MSD)* ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 13 ya mwaka 1993.

Majukumu makuu ya *MSD* ni matatu ambayo ni:-

(i) Kuagiza dawa na vifaa tiba;

(ii) Kutunza dawa na vifaa tiba; na

(iii) Kusambaza dawa na vifaa tiba kwa walengwa ambao ni vituo vya kutolea huduma za afya vya umma hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya inapeleka fedha *MSD* kila robo mwaka kwa ajili kutoa huduma, dawa na vifaa tiba kwa hospitali kulingana na mahitaji na kusambaza masanduku ya dawa katika Zahanati na Vituo vya Afya. Fedha hizo huingizwa kwenye *accounts* za hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Serikali na hospitali teule.

Wizara ya Afya inapitisha fedha *MSD* ili fedha hiyo itumike kwa madhumuni yalikusudiwa kwa nia ya kuboresha huduma za afya hususani upatikanaji wa uhakika wa dawa na vifaa tiba vyenye ubora unaokubalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vituo vinavyopata fedha za kununua dawa na vifaa tiba kupitia *MSD* pia vina vyanzo vingine vya mapato kutokana na sera ya uchangiaji wa huduma za afya. Fedha inayopatikana na inabakia katika vituo hivyo kuviwezesha kununua dawa na vifaa tiba nje ya *MSD* vinapokosekana.

Mheshimaiwa Spika, vyanzo hivyo ni pamoja na *Capitalization of Hospital Pharmacies* ambapo hospitali zinatoa dawa kwa wagonjwa kwa asilimia hamsini ya bei ya kununulia dawa *MSD,* Bima ya Afya *(National Health Insurance Fund),* Mfuko wa Afya ya Jamii *(Community Health Fund)* na Uchangiaji wa huduma ya afya vituoni yaani *User Fees.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ununuzi wa dawa na vifaa nje ya *MSD* unatakiwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi ya mwaka 2001yaani *The Procurement Act.*

Mheshimiwa Spika, wakuu wa vituo vya kutolea huduma za afya wanatakiwa kusimamia matumizi ya fedha yanayopatikana na vyanzo vilivyotajwa hapo juu kwa nia ya kuboresha huduma za afya katika vituo vyao. Aidha, wakuu wa vituo wanashauriwa kuwa na mawasiliano ya karibu na *MSD* ili kuwawezesha kuagiziwa dawa na vifaa kufanyika mapema ili kuepukana ukosefu wa vifaa hivyo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wanafanya, lakini kazi hii nzuri ambayo imewezesha fedha nyingi kuja kwenye Halmashauri kwa ajili ya ununuzi hasa wa vifaa vya Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, unakwamishwa na ukiritimba ulioko kule *MSD.* Mara nyingi wanakuwa hawana vifaa au wanavyokuwa navyo vinakuwa na ubora hafifu ama ni vya bei kubwa.

Je, Mheshimiwa Waziri atasaidiaje kuhakikisha kwamba *MSD* inatoa ruhusa kwa Halmashauri zetu kuweza kununua vifaa nje ya *MSD.* Kwa sababu ruhusu hiyo wana ukiritimba nayo hawatoi hata kama hawana vifaa, wanakuwa wagumu kuruhusu vifaa hivyo kununuliwa mahali pengine?

Je, Serikali ina mipango gani ya ujumla ya kuimarisha utendaji kazi wa *MSD?*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Ni kweli anayozungumzia Mheshimiwa Job Ndugai ni historia ya huko nyuma ya *MSD* ya vifaa hafifu, bei kubwa na wakati mwingine kukosekana ni historia iliyokuwepo. Jambo hili sasa limerekebishwa. Kwanza, hospitali zinaruhusiwa kama wanakihitaji kifaa maalum wafanye *order,* waseme sisi katika fedha hizi sisi tunataka kifaa fulani na kinaagizwa maalum kwa wale watakaoagiza.

Pili, siku hizi ina mtindo wa *indent system* baadhi ya hospitali zetu zinaagiza dawa kutokana na mahitaji yao. Kwa hiyo, pale si mahali ambapo utaweka tu dawa kungojea neno ni mahitaji. Kwa hiyo, tunaomba *order* zifanyike. Sasa kuna wenzetu wengine wanaofanya shughuli hii pia wanayo matatizo kwa mfano mimi nimezunguka sana na napeleleza na naambiwa tatizo hili lipo.

Mheshimiwa Spika, nimewaambia nionyesheni hicho kifaa mlichonunua kutoka *MSD* twende bega kwa bega mpaka *MSD* tukawadai kwa nini wamewauzia hiki kifaa hafifu. Tumekuta vitu vingi ni vya miaka ya nyuma kabla jambo hili halijarekebishwa.

Kwa hiyo, mimi ninakuhakikishia Mheshimiwa Job Ndugai kwamba *MSD* ina mpango kurekebisha *MSD* ifanye kazi kwa ufanisi . Kwa bahati mbaya sana wakati tunapopata matatizo ya fedha, *MSD* wanatoa dawa kwa mkopo. Hivi sasa *MSD* ina deni katika Serikali shilingi bilioni 11 kwa hiyo na wao wanakuwa na tatizo la kuendeleza huduma bora. Lakini nataka tu nihakikishie kabisa Bunge kwamba *MSD* inafanya kazi

nzuri sana na kwamba kama wakipata ushirikiano, *MSD* itafanya kazi bora na vifaa vya *MSD* ni rahisi kwa kuwa wao wanasamehewa kodi kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kupata nafasi na nafurahi pia kwa majibu mazuri sana ya Waziri wa Afya. Lakini ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la *MSD* ni kama ilivyosemwa ni ukiritimba; na kwa kuwa Sheria iliyounda *MSD* ilikuwa imetungwa mwaka 1993 wakati kulikuwa hakuna hii Sheria ya *Government Agencies.* Kwa sababu sasa kuna mfumo wa *Government Agencies* ili kuongeza ufanisi katika *MSD,* kwa nini Serikali haifikirii uwezekano wa kuirudisha kwenye *Government Agencies* au kuunda chombo kingine ambacho kitashindana na *MSD* ili dawa zipatikane maana yake ni kweli matatizo yapo ya upatikanaji wa dawa kutoka *MSD?*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Henry Shekiffu, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ama kwa hakika *MSD* ni *Government Agencies* ya kuagiza na kusambaza madawa. Ila hatuiiti tu *Agents* lakini wao walianza kazi hii mapema hata kabla ya *Agencies* zingine.

Swali la ukiritimba, tusipoangalia tukaruhusu watu wachukue hela za Serikali kwenda kwenye maduka yoyote tu kwa dawa zinazopatikana huo ndio mwanzo wa ubadhirifu. Huko ndiko tulikotokea kabla ya Sheria hii ndivyo ilivyokuwa katika maeneo mengi siyo tu kwa dawa, hata kwa vifaa vingine vya Serikali vinanunuliwa visivyokuwa na ubora unaostahili. Kwa hiyo, hapa ni mahali pa kuhakikisha ubora. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Wizara yake imejitahidi sana kuhakikisha *MSD* inafanya taratibu sahihi. Lakini kwa kuwa bado kwenye uduni wa vifaa kwa mfano, *BP machine,* zinaharibika hata mwezi haufiki imeshaharibika. Unajikuta mpaka *labour ward* hakuna *BP machine, forces* zinavunjika hovyo, *thermometer* unatingisha ili ku-*reduce mercury* inavunjika wakati unatingisha.

Je, Mheshimiwa Waziri atatusaidia vifaa hivi viweze kupatikana vyenye ubora unaotakiwa?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr.Zainab Gama, swali lake kama ifuatavyo:-

Suala la kuvunjika kwa vifaa kila kiwanda kinajua *rate* ya *breakages.* Kinapotengeneza vitu kuna *rate* ya *breakages* lakini kama hivi vitu vinasemekana kwamba kikitumika tu kinavunjika. Mimi nasema yule aliyenunua ana wajibu wa kulalamika vile vile ili tulifuatilie. Lakini tukingojea kuja mpaka hapa tunalieleza hili, tutakuja pengine ni matumizi mabaya vile vile katika maabara ya vifaa hivyo. Tusisahau vile vile kwamba vifaa hivi havitumiki tu hospitalini, tunajua kama vingine vinatumika huko nje vile vile. *(Makofi)*

Na. 7

**Hali ya Viwanda Nchini**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI (k.n.y MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA)** aliuliza:-

Je, tangu Serikali ichukue hatua ya kubinafsisha viwanda ni viwanda vingapi vinafanya kazi na vingapi havifanyi kazi hadi sasa na ni vingapi vimejengwa?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Tangu Serikali ichukue hatua ya kubinafsisha viwanda, viwanda ambavyo vimebinafsishwa na vinafanya kazi ni 55 ikiwa ni pamoja na viwanda vya nguo mfano, Urafiki, *Namera Group of Industries* yaani zamani ilikuwa *Sunguratex, Kiltex* Arusha, *Morogoro Canvas, Mwatex, Polytex* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vya vinywaji mfano, *Tanzania Breweries, Tanzania Distilleries Ltd., Dar Brew Ltd., (Kibuku)* na kadhalika, viwanda vya saruji mfano, *Tanzania Portland Cement, Mbeya Cement* na *Tanga Cement.* Viwanda vya chuma mfano, *Steel Rolling Mill* na viwanda vya usagishaji wa nafaka mfano, viwanda vilivyokuwa vya *National Milling Corporation* na viwanda vya sabuni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, viwanda ambavyo vimebinafsishwa lakini havifanyi kazi ni *Morogoro Tanneries, Tanzania Tanneries* Moshi, *Mwanza Tanneries, Ubungo Spinning, Ubungo Garments, Tanzania Bag Corporation, Light Source Manufactures Ltd.* na *Morogoro Shoe Ltd.* ambacho kiliungua moto.

Aidha, vipo viwanda ambavyo ukarabati uliendelea ili kuweza kuanza uzalishaji na baadaye kufungwa kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha za kununua mitambo mipya kwa ajili ya ukarabati *(modernisation)* kuweza kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika soko. Mfano ni kiwanda cha *Ubungo Spinning Milling.*

Kuhusu viwanda vilivyojengwa katika kipindi cha mwaka 1995 - 2004 ni pamoja na viwanda vya nguo yaani mfano, *NIDA Textile Mills, Star Apparel Ltd, African Pride Textile Mills, Lakhani Textile Ltd. Karibu Textile* na kadhalika.

Viwanda vya Mafuta ya kupikia mfano, *BIDCO Ltd,* ambacho kiko Mikocheni, *Best Tigra Ltd.,* kiko *Mbagala Murzah Oil Mills Ltd.,* ambacho kiko *Pugu Road* au *Mwalimu Nyerere Road.* Viwanda vya chuma mfano, *Sita Steel Rolling Mill, Hans, Nail*

*Manufactures, Trishala Rolling Mills* vyote viko Arusha. *Nyakato Steel Mills* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wizara inafanya mazungumzo na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(National Bureau of Statistics)* ili kufanya sensa ya viwanda kwa lengo la kupata taarifa kamili za viwanda vyote nchini ikiwa ni pamoja na vipya vilivyojengwa. Sensa kama hiyo kwa mara ya mwisho ilifanyika mwaka 1989.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu langu, ninayo orodha ndefu ya baadhi ya viwanda vilivyofufuliwa baada ya kubinafishwa na vipya vilivyojengwa katika kipindi cha mwaka 1995 - 2004 ambayo sikuweza kuingiza katika jibu hili. Niko tayari kumpatia Mheshimiwa Mbunge taarifa hiyo kama atapenda.

**MHE. PROF. SIMON N. MBILINYI:** Ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Shida ya Dr. Lawrence Gama, ni kwamba tangu Uhuru hakijajengwa kiwanda hata kimoja pale Songea. Nafikiri kuwa kuna mpira kati ya wawekezaji viwanda na umeme. Watu wa umeme wameshindwa kupeleka umeme Songea kwa hivyo watu wa viwanda au wawekezaji wanaona ni vigumu kwenda kuweka viwanda kule.

Je, Wizara hizo mbili zinawasiliana kwa muda unaokuja ili wapate viwanda kule Songea?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Songea haijapata bahati ya kupata kiwanda kutokana na tatizo la umeme. Lakini suala la umeme sasa hivi tunalifanyia kazi nzuri nalo litakuwa ni umeme unaotokana na mkaa wa mawe pale Mchuchuma. Yeye Profesa Simon Mbilinyi kama Mwenyekiti wa *NDC,* suala hili analielewa na sisi Serikali tumelivalia njuga kwamba umeme wa Mchuchuma unaotokana na makaa ya mawe utaweze kutumika nadhani katika mwaka 2007/2008. Kwa hiyo, tukifika hapo tutaweza kupeleka umeme Songea na hivyo kuwawezesha wao kupata kiwanda. *(Makofi)*

**MHE. *MAJOR* JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kiwanda cha *Kibo Breweries* cha Moshi kilibinafsishwa na mwekezaji huyu ametelekeza kiwanda hicho na hivyo kukosesha Serikali mapato na ajira pia. Je, Wizara ya Viwanda na Biashara kama mwenye dhamana ya Serikali, atachukua hatua gani kuhakikisha kwamba mwekezaji amefufua kiwanda hicho na kutekeleza lengo lililokusudiwa na Serikali la ubinafsishaji?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa *Major* Mstaafu Jesse Makundi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kiwanda cha Kibo cha Bia kilijengwa na mwekezaji binafsi kutoka Kenya ambaye hakuweza kuhimili ushindani katika soko la bia nchini Tanzania. Kwa hiyo, akakubaliana akiuze kiwanda hicho kwa *Tanzania Breweries Ltd.,* ambao wao wenyewe wanasema hivi kama *East African* na *Breweries* ambayo iko Kenya wameshindwa kukiendesha kiwanda hiki wao hawataweza kukiendesha kwa tafsiri ya kuajiri watu na kuendesha kiwanda isipokuwa wataendelea kutengeneza bia ambazo zilikuwa zinatengenezwa na *Kibo Breweries.* Kwa hiyo, wateja wa Tanzania wataendelea kunufaika na bia ambayo ilikuwa inatengenezwa na *Kibo Breweries* isipokuwa hawataendelea kuajiri watu kufanya kazi pale kwa sababu uwezo wa namna hiyo kwa kuzingatia faida ilikuwa haiwezekani.

Lakini pili, kwamba Serikali imekosa mapato si kweli mapato ambayo yanatokana na kodi kutoka kiwanda cha *Tanzania Breweries* ni kubwa sana. Sasa hivi hapa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 11 katika miaka ile 1997/1998 mpaka shilingi bilioni 55 katika mwaka 2003. Kwa hiyo, faida imeongezeka na malipo yao ya mapato kwa kupitia kodi kwa Serikali, ni kubwa zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Na. 8

**Ujenzi wa Sekondari Kupitia Mpango wa *MMES***

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Kigoma Ujiji ni mmoja kati ya miji michache Tanzania yenye shule chache za Sekondari na kwa kuwa hata Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa amelithibitisha hili kupitia hotuba yake kwa Taifa ya mwisho wa mwezi Oktoba, 2004 kwa kusema kuwa kutopata fursa ya kutosha kupata elimu ya Sekondari hasa kwenye yale maeneo yenye Sekondari chache kama yale ya Mji wa Kigoma Ujiji kutapelekea kukosekana watu wenye sifa za kupata ajira. Serikali na kwingineko hivyo kuwafanya watu wa maeneo hayo kutowakilishwa vizuri kwenye masuala ya Kitaifa:-

(a) Je, Serikali imepanga kujenga shule ngapi za Sekondari za Darajaa la *O* na *A* kupitia mpango mzima wa *MMES?*

(b) Je, Serikali inasemaje kuhusu kuendelea kuizuia shule iliyokuwa ya Ubalozi wa Kongo ambayo sasa baada ya kufuata ushauri wa Waziri wa Elimu na Utamaduni wa kubadili umiliki huo kwa Watanzania lakini bado haijafanywa hivyo hivi tatizo hasa ni nini?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga katika mpango mzima *MMES* 2004 - 2009, kujenga shule mpya za Sekondari 1,500 kwa lengo la kutoa elimu ya Sekondari kwa 50% ya rika lengwa la elimu hiyo. Lengo la mwaka wa 2004/2005 ni kuongeza nafasi za Sekondari hadi kufikia 35% ya watahiniwa wa darasa la saba wa mwaka 2004 kujiunga na Kidato cha kwanza mwaka 2005 Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya.
Aidha, 35% ya watahiniwa wa kidato cha nne kujiunga katika kidato cha tano.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kila Wilaya inapewa ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya kuchangia kwenye nguvu za wananchi katika ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu ili kufikia lengo hilo la mwaka huu. Kila Wilaya imepangiwa idadi ya madarasa kulingana na vigezo hivi vitatu:-

(i) Idadi ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba mwaka 2004.

(ii) Nafasi za kidato cha kwanza walizonazo tayari ndani ya Wilaya hiyo.

(iii) Nafasi walizopangiwa Kitaifa ili waweze kufikia *transition rate* hiyo ya 35%.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kigoma Mjini imepangiwa ruzuku ya ujenzi wa madarasa saba ili kuweza kufikia lengo hilo la kupeleka Sekondari 35% ya watahiniwa wa darasa la saba mwaka jana. Umuhimu wa kwanza ni kuongeza tu madarasa kwenye shule zilizopo za Serikali zilizojengwa na wananchi. Umuhimu wa pili ni kujenga madarasa ya shule mpya.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haizuii shule iliyokuwa ya ubalozi wa Kigoma, *Kigoma Congolese Secondary School* kumilikiwa na Watanzania. Kinachotakiwa ni anayeomba kuwa mwenye shule na *manager* wa shule atimize masharti ya usajili ikiwa na pamoja na kutoa elimu kwa kutumia lugha zinazoruhusiwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo tuliyoipitisha mwaka 1995 ambazo ni lugha ya Kiswahili kwa elimu ya awali na elimu ya msingi na lugha ya kiingereza kwa elimu ya sekondari. Ingawa somo la Kifaransa linaweza kufundishwa kama mojawapo ya masomo ya kuchagua yaani *optional subject.*

Aidha inatakiwa shule hiyo ifuate mitaala ama ya Tanzania au ya Kimataifa kama usajili wake utakuwa umetimiza mashariti ya usajili wa kuwa shule ya Kimataifa.

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Waziri ametoa takwimu inayoitwa *transition rate* katika mpango huu *MMES* sijui anafikiriaje kauli ya Rais kuhusu shule hizi zijengwe kwa uwiano kwa sababu kama *transition rate* ya watu wenye shule 200 itakuwa sawa sawa na *transition rate* ya watu wenye shule kumi uwiano huo utafikiwa ?

Mheshimiwa Spika, pili ningependa kujua kama habari alizosema Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni kuhusu hii *Francophone school* ya kule Kigoma Ujiji walikwishazifikisha kwa wahusika ili watekeleze matakwa haya au ni maneno yanayosemwa leo wakati wahusika wenyewe hawajaambiwa chochote? Ahsante Mheshimiwa Spika.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Kuhusu uwiano kama nilivyosema katika kujibu swali la msingi tunachoangalia ni watahiniwa wa darasa la saba kwa hiyo, kama Wilaya inalenga kuwa na sekondari nyingi. Jambo mojawapo ni kuhakikisha kwamba watoto wote wa miaka saba wanajiunga darasa la kwanza na hawaachi shule mpaka wafike darasa la saba ili asilimia yenu wale wanaotokana na hiyo asilimia 35 wawe wengi zaidi.

Kwa hiyo, kweli changamoto kubwa ni kusimamia mambo yote muhimu katika mlolongo wa elimu kuanzia darasa la kwanza na kutokuacha shule mpaka wafike darasa saba ili wawe wengi ili *percent* ile iweze kutoa nafasi nyingi, kama kila wilaya itafanya namna hiyo na tutakwenda kwa asilimia hiyo hiyo katika kila Wilaya uwiano huo unakuja *automatically* unajitokeza wenyewe kwa sababu tunagawa kwa usawa kwa kufuata wingi uliopo. Hatuwezi tukasema tunafuata usawa kwa kufuata kila Wilaya tunafuata wingi wa watoto katika Wilaya hiyo watoto waliozaliwa wakaenda shuleni wafike darasa la saba, mimi ninahakika tutafikia huo uwiano.

Kuhusu swali la pili ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tulipokea maombi kutoka kwa wanaotaka kumiliki shule hiyo. Lakini makosa waliyofanya na hata usajili hatukuweza kuutoa ila tumewapa ushauri ni waliomba kuendesha shule hiyo kwa lugha ya kifaransa na walitaka kufuata Mitaala ya nchi jirani. Sasa utaratibu wetu kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo, mitaala lazima iwe ama ya Tanzania au mitaala inayotambulika ya Kimataifa kama shule imeomba usajili wa Kimataifa na wameandikiwa barua na Afisa Elimu Kiongozi na nina hakika wako katika jitihada ya kutimiza mashariti hayo na Mheshimiwa Mbunge akiwashauri waje ndani ya utaratibu, usajili hautakuwa na kikwazo chochote.

Na. 9

**Kufutwa Kwa Baadhi Ya Michepuo Ya Masomo Katika Sekondari Nchini**

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza:-

Kwa kuwa imefahamika kuwa Serikali inafuta michepuo kadhaa katika shule za Serikali kuanzia mwaka 2004:-

(a) Je, kuna ukweli gani kuhusu taarifa hizo na ni michepuo ipi iliyofutwa?

(b) Je, ni shule zipi hasa zimeathirika au zimehusika katika zoezi la kufutiwa michepuo hiyo; na ni sababu gani za msingi zilizosababisha Serikali kuchukua hatua hatua hiyo?

(c) Je, ni athari gani zitakazotokea kwa vifaa hasa vile vya ufundi iwapo michepuo hiyo imefutwa na shule za ufundi kwa sasa zina vifaa vyenye jumla ya thamani gani kwa kuorodhesha kwa kila shule?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyolitaarifu Bunge hili katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu Serikali kupitia Wizara yangu imeamua kupunguza masomo ya Sekondari kutoka 13 hadi nane. Masomo mahususi yaani *core subjects* yatakayofundishwa ni Hisabati, Kiswahili, Kingereza, Baolojia, Fizikia pamoja na Kemia, Historia, Uraia na Jiografia. Michepuo iliyofutwa ni ile ya kilimo, Ufundi na Biashara. Michepuo hiyo ina vyuo vyake chini ya Wizara husika lakini mitaala ya masomo hayo imerekebishwa ili masomo hayo manane yanayofundishwa yawe pia ni masomo chukuzi au masomo bebezi kwa lugha ya kiingereza *carrier subjects* ya mada muhimu za elimu ya kujitegemea, zilizokuwa kuwa katika ya michepuo.

(b) Mheshimiwa Spika, shule zilizohusika katika zoezi hili la kufutiwa michepuo hiyo ni zile zote zilizokuwa na michepuo ya Ufundi, Kilimo na Biashara. Serikali ilifikia uamuzi huo kwa sababu ya kuwa na uwiano unaofaa baina ya malengo ya elimu ya kuhitimu ngazi husika na malengo ya kuendelea katika ngazi ya juu inayofuata. Wakati huu ambapo tumeamua kuongeza nafasi za sekondari ya ngazi ya kawaida yaani kidato cha kwanza hadi kidato cha nne na ngazi ya juu kidato cha tano na kidato cha sita, kwa nia pia ya kuongeza nafasi za elimu ya juu imelazimiaka kuongeza ubora wa elimu ya sekondari katika masomo mahususi ya ngazi hiyo ya elimu ya sekondari ni kwanza Hisabati, pili Lugha na kwa maana ya kwetu sisi hapa ni lugha za Kiswahili na Kiingereza, tatu masomo ya Sayansi kwa maana ya Baolojia, Fizikia na Kemia na nne Maarifa ya Jamii kwa maana ya Historia, Jiografia na Uraia.

Kutokana na kufutwa michepuo, vipindi vya masomo haya mahususi vimeongezwa na mitaala imeboreshwa ili masomo haya yawe pia ni masomo chukuzi ya elimu ya kujitegemea na masuala mtambuka yaani *cross cutting issues* hususani ya Mazingira, Afya ya Jamii na Teknolojia ya Mawasiliano.

(c) Mheshimwa Spika, hakuna athari yoyote itakayotokea kutokana na kufutwa michepuo hii katika shule za sekondari kwa sababu vifaa vilivyopo tayari vimechakaa sana na katika shule nyingine havitumiki kabisa. Vifaa vingi vilivyopo vilinunuliwa miaka ya 1970 na havijawahi kubadilishwa wala kufanyiwa matengenezo. Kwa hiyo, thamani yake kimahesabu haipo kwa sababu muda wake umekwisha. Lakini pale ambapo baadhi ya vifaa bado vinaweza kutumika, vitaendelea kutumika katika vitengo vya

matengenezo na ukarabati wa majengo ya shule kwenye kanda husika. Utaratibu huu wa masomo manane umeanza kutumika Januari, 2005 kwa kidato cha kwanza tu. Wakati kidato cha pili hadi cha nne wataendelea na masomo wanayoyasoma hadi watakapomaliza kidato cha nne.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake lakini ningependa kufahamu kwa kina, nchi yetu inapiga vita umaskini na masomo ambayo yangesaidia sana kupiga vita umaskini ni pamoja na kilimo, ufundi na biashara, kwa kuwa vijana wetu wengi hawaendelei baada ya masomo ya sekondari kuingia kwenye hivyo vyuo vingine ambavyo amevitaja Mheshimiwa Waziri, sasa je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kufuta michepuo hiyo ni kurudi nyuma katika azma yetu ya kupiga vita umaskini?

Pili, Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba bado wanafanya tathmini ya vifaa vilivyokuwepo katika shule hizo, Mheshimiwa Waziri ningependa anihakikishie kwamba vifaa hivyo viko salama na kuna chombo mahususi kimeundwa ili visiende katika mikono ya watu binafsi kwa sababu taarifa tuliyonayo ni kwamba sasa vimeanza kuchangamkiwa maeneo fulani na huenda visiende tena kule ambapo vinakusudiwa kama alivyosema. Ana uhakika gani kwamba kuna chombo kinasimamia na inategemea jinsi uamuzi ulivyopitishwa bila kwanza kuweka chombo hicho mahususi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, maswali yake kama ifuatavyo: -

Kwanza kwamba nchi yetu tunapiga vita umaskini na labda kuondoa michepuo basi ndiyo tumeacha kazi hiyo, tumeacha kufundisha vijana wetu elimu inayohitajika watakapo maliza shule, ufundi unaohitajika masuala ya kilimo.

Napenda nimrejeshe kwenye jibu langu la msingi kwamba zile mada za elimu ya kujitegemea ambazo zilikuwemo katika masomo haya ya ufundi sasa zimeingizwa kwenye masomo yale mahususi na nikaeleza kwamba masomo hayo ni masomo chukuzi ya mada hizo. Kwa hiyo, siyo kwamba tumeacha kufundisha labda nimweleze kwa kutoa mifano, kwa mfano mada za masomo ya kilimo zimeingizwa katika masomo ya Baolojia na katika masomo ya Jiografia.

Katika Jiografia tunajifunza ukanda unaofaa kwa mazao yapi na katika Baolojia tunafundisha Sayansi ya Kilimo vitu kama *photosynthesis* na kadhalika ili tuweze kufundisha vizuri hata maua wanayojifunza shuleni badala ya kujifunza ua lile tu la *hibiscus* ambalo ndilo linajulikana kama *complete flower* tuliyojifunza sisi wengine watafundishwa pia maua ya mazao yale wanayoyalima kama vile maharagwe, mahindi, *cross pollination* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeingiza katika masomo hayo, mchepuo wa biashara ingawaje hatutaufundisha mchepuo wa biashara lakini katika hisabati limeimarishwa somo la mada za hesabu za biashara zinazojulikana kama *commercial arithmetic.* Kwa hiyo, si kwamba tumeacha kufundisha, yale mambo muhimu yatafundishwa katika masomo hayo chukuzi.

Mheshimiwa Spika, pili, mimi sikusema kwamba bado tunafanya tathmini, nilichosema ni kwamba sehemu kubwa ya vifaa hivyo vimechakaa na havifai kutumika. Lakini nimesema vile ambavyo vinafaa ambavyo rekodi yake tunaijua kabisa kwa sababu iko katika vitabu vya Serikali vitaendelea kutumika katika vitengo vya matengenezo vya *school maintenance* na kusaidia ujenzi kwa shule hizi nyingi ambazo tunaendelea kuzijenga.

Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba usimamiaji kwamba hakuna uvujaji ama vifaa hivyo kupelekwa katika maeneo yasiyohusika tutazingatia na kama Mheshimiwa Mbunge anayo habari yoyote ile kwamba kuna taarifa ya kutaka kupora baadhi ya vifaa hivyo namwomba anitaarifu ili tushirikiane kuchukua hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, dakika tano za swali hili moja zimekwisha, vema kama kuna hamu ya kuuliza maswali nitatoa nafasi zaidi ili mengine yachelewe. Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilombai atafuatia na Mheshimiwa Dr. William Shija.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali katika hili, hili suala ni nyeti na ni zito na linaigusa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuondoa somo, kulipunguzia muda maana yake kijana anayejifunza atakapoenda juu hatakuwa na ujuzi sawa na yule aliyepata muda wa kutosha. *(Makofi)*

Kwa kuwa sasa hivi tunafungua vyuo vikuu vya masomo haya na maana yake vitapokea wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuweza kwenda vizuri kwa hiyo hatutakuwa na wataalam, je, Mheshimiwa Waziri anakubali suala hili kwa kuwa ni nyeti lirudi kwenye Kamati ya Huduma za Jamii lijadiliwe upya? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda tufahamu na tuzingatie baadhi ya mabadiliko ambayo tumeamua kuyafanya kwa mfano tumeleta Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari, chini ya mpango huo tunaongeza kwa kiwango kikubwa sana kufikia asilimia 50 wanafunzi watakaosonga mbele na elimu ya juu. Kwa hiyo, mabadiliko haya tunayoyafanya yanazingatia tuwe na uwiano mzuri kati ya wanafunzi ambao wako katika sekondari kwa maana ya kwamba wanahitimu ngazi hiyo na hawatasonga mbele. Tuwe na uwiano mzuri baina ya kundi hilo ambalo halitasonga mbele ambalo kweli unataka lijue masuala ya elimu ya kujitegemea kwa maana ya kwamba wataingia katika jamii. Lakini tuwe na uwiano mzuri na mahitaji ya elimu ya juu huko katika miaka iliyopita wanaosonga mbele walikuwa

wanakuwa asilimia 15, 20 sasa tutawafikisha asilimia 50 wanaokwenda kidato cha tano na cha sita na wanaokwenda ngazi ya Chuo Kikuu kwa hiyo, unahitajika pia uwaimarishe katika masomo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa kuzingatia kuleta uwiano kati ya mahitajio hayo mawili wataalam wanaita *terminal objectives of education* na *progression objectives of education* lazima kila wakati uwe na *balance* nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi sina wasiwasi kabisa kama Kamati ya Huduma za Jamii watataka tulichambue jambo hili vizuri zaidi niko tayari kufanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuhahidi Mheshimiwa Dr. William Shija, uliza swali lako.

**MHE. DR. WILLIAM F. SHIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ndogo hii niulize swali moja la nyongeza, nimetiwa moyo sana na majibu ya Mheshimiwa Waziri aliyoyasema hapo mwishoni na kwamba je, kwa kuwa suala la elimu kwa Taifa na hata kwa Bara letu la Afrika sasa ni nyeti na ni zito kama wenzangu walivyosema Waziri na Serikali atakubaliana na mimi kwamba ni vizuri kuwauliza wadau kikamilifu juu ya mabadiliko yoyote yanayostahili kuwekwa katika mitaala na suala zima la elimu ya Taifa kwa sababu sisi Tanzania tunahusiana na watu wengine vile vile. Waziri atakubaliana na mimi kwamba tusifanye mabadiliko mpaka tunapokamilisha kuuliza wadau wote katika suala la elimu? Akikubaliana na mimi hivyo nitashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, maswala ya elimu, suala zima la elimu kwa watoto wetu ni muhimu sana kwa maendeleo yao na maendeleo ya nchi na mimi nakubaliana nayo kabisa na ninapenda nimhakikishie kwamba mitaala hii iliyotazamwa upya kwa malengo haya nimetoka kuyaeleza ambayo amesema anakubaliana nayo. Haikuendewa haraka haraka hata kidogo tofauti na ambavyo wamekuwa wakiandika watu katika baadhi ya magazeti. Jambo hili limefanyiwa uchunguzi wa kina na chombo maaalum, Taasisi ya Elimu Tanzania na wanapofanya kazi hiyo Taasisi ya Elimu Tanzania hushirikisha wadau wote na hata mimi mwenyewe jambo hili sijalifungia tu kwamba nimelifanyia maamuzi.

Mheshimiwa Spika, napenda nikumbushe kwamba katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka huu katika *paragraph* ya 18.12 ukurusa wa 26 na nukuu nilivyolitaarifu Bunge hili ili lifahamu, nilisema: "Kupunguza masomo ya sekondari kutoka 13 kuwa manane yakiwemo *Mathematics,* Lugha (Kiswahili na *English)* Masomo ya Sayansi *(Biology, Physics* na *Chemistry)* na Sayansi ya Jamii *(History, Geography* na *Civics)* na kuacha kufundisha masomo ya michepuo *Technical Studies, Agriculture* na *Commerce* ambayo yana vyuo vyake chini ya Wizara husika. Kwa hiyo, haiwezi ikasemwa jambo hili nimelificha, nimeliweka wazi mbele ya Bunge hili, limejadiliwa na Bajeti yangu ilipitishwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nimeambiwa hili ni swali nyeti, kuna mwingine anataka kuuliza.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kinachozungumzwa hapa pamoja na majibu ya Waziri ni ushirikishwaji wa wadau wa sekta ya elimu. Tunafahamu wote kwamba kuna Taasisi ya Elimu ina watendaji wa Serikali ambao wanapokea maagizo ya Serikali. Tulichosema ambacho wenzangu wamekizungumza je, Waziri yuko tayari kuwashirikisha wadau wa sekta ya elimu waweze kuchangia kwenye tatizo hili la kuondoa baadhi ya masomo ya msingi ambayo watu wanalalamikia?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, labda nirudie kusema tena kwamba ushirikishwaji umefanyika kwa kiwango kikubwa sana na waandaaji wa mitaala chombo ambacho Bunge hili lilipitisha sheria ya kuunda Taasisi ya Elimu Tanzania ndicho chombo kilichofanya uchambuzi wa mitaala na kimefanya kwa utaratibu shirikishi kabisa na mimi kama Waziri ninayesimamia nimeridhika kabisa kwamba ushirikishwaji ulifanywa kwa mapana na marefu.

Lakini narudia tena kwamba suala la elimu huwezi ukasema umefikia mwisho na uboreshaji wa mitaala ni *continuous process,* ni jambo linaloendelea. Kama kuna kundi lolote wanataka kutoa mawazo zaidi pamoja na Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii mimi niko tayari kwa sababu nitakuwa nanufaika na mawazo ya wadau pamoja na Wabunge wenzangu. *(Makofi)*

Na. 10

**Mahitaji ya Mbolea Vyanda za Juu Kusini**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakulima wa Nyanda za Juu Kusini ikiwapo Mkoa wa Mbeya inategemea sana mbolea za viwandani katika kilimo na kwa uzoefu wa mwaka 2003 mbolea hizo zilichelewa sana kufika Mbeya;

(a) Je, Serikali imejiandaa kwa kiasi gani kwa msimu ujao 2004/2005 ili mbolea hizo ziweze kupatikana kabla ya Septemba, 2004?

(b) Serikali haioni kuwa ipo haja ya kutoa ruzuku ya uhakika badaya ya tofauti ya shilingi 500/= hadi 1,000/= na ile ya wafanyabiashara wa kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, naomba kutoa maelezo machache ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mvua za Nyanda za Juu Kusini huanza kunyesha katikati ya mwezi wa Novemba na kuendelea hadi Aprili au Mei ya mwaka unaofuata. Kinachotakiwa kwa hiyo, ni kufikisha mbolea za kupandia kwa wakulima kabla ya tarehe 10 Novemba. Mbolea za kukuzia zinatakiwa ziwafikie wakulima mwanzo wa mwezi wa Januari na ziendelee kupatikana hadi mwezi wa Machi. Kupeleka mbolea mapema sana kabla ya msimu, kwa mfano Septemba, kutawaingiza wasambazaji gharama na pengine hata hasara.

Mheshimiwa Spika, japokuwa mwaka wa 2003/2004 ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa mpango wa kutoa ruzuku kwa mbolea, upelekaji wa mbolea kwenye mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ulikuwa wa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maelezo haya mafupi sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benson Mpesya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ili kuhakikisha kwamba usambazaji wa mbolea unafanyika kwa wakati muafaka na kwa ufanisi, Wizara iliandaa utaratibu ufuatao:-

(1) Nilitenga jumla ya shilingi bilioni 7,244 katika Bajeti ya mwaka wa 2004/2005 ili kufidia sehemu ya gharama ya usafirishaji wa mbolea.

(2) Iliteua 14 vya kusambazia mbolea mikoani.

(3) Ilisimamia uundaji wa Kamati za Mikoa na Wilaya za kuratibu na kutathmini usambaji wa mbolea.

(4) Ilifanya vikao na waingizaji wa mbolea kati ya tarehe 18 Juni, 2004 na 27 Oktoba, 2004. Kati ya Julai na Oktoba *TFC* ilipeleka Mbeya mbolea ya *CAN, Urea* na *DAP.* Mwezi wa Novemba makampuni ya watu binafsi yalipeleka Mbeya mbolea ya *DAP* na *Urea.* Ilipofika Oktoba, 2004, Mkoa wa Mbeya ulikuwa umepokea tani 3,656 za *DAP* na tani 2,004 za *Urea.* Hivyo, kufikia Januari, 2005 jumla ya tani 5,615 za *DAP* na tani 10,418 za *Urea* zilikuwa zimefikishwa.

(b) Ruzuku ya mbolea iliyopangwa na Serikali katika mwaka wa 2004/2005 ilipunguza bei ya mbolea kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, *DAP* iliuzwa kwa shilingi 14,000 kwa mfuko katika vituo vikuu badala ya shilingi 26,814/= katika soko. Aidha, *Urea* inauzwa kwa shilingi 14,000/= badala ya shilingi 21,314/=. Hivyo, ni dhahiri kuwa ruzuku iliyotolewa katika vituo vikuu ni kubwa kuliko alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na vile vile pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara kuhakikisha kwamba mbolea zinafika kwa wakati, jambo ambalo wananchi wamelifurahia sana na kuipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Nina swali dogo la nyongeza la kutaka kuboresha hali hiyo.

Kwa kuwa katika mbolea zote, mbolea aina *CAN 26* bado inauzwa katika kiwango cha shilingi 19,500/= mpaka sasa hivi. Wafanyabiashara wanadai kwamba hiyo si mbolea ambayo imepewa ruzuku naomba Wizara itufafanulie hali hiyo ikoje kwa maana kuwepo kwa mbolea kutasaidia kabisa katika kuhakikisha wananchi wanaweka na mazao wanapata kwa wingi? Naomba ufafanuzi kuhusu mbolea ya *CAN*.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NACHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa pongezi, kwa kazi hiyo tuliyokwisha ifanya.

Pili, ningependa kujibu swali kuhusu bei ya mbolea katika Mikoa hiyo aliyoitaja hususani wa Mbeya, kuwa *CAN* nayo imo katika kupunguzwa kupata ruzuku kwa mfano kwa kiasi cha asilimia 75, sasa nilikuwa natafuta tafuta hapa kuona hasa hasa kwa kituo kile. Lakini kwa mfano ile iliyokwenda Makambako na ile iliyokwenda Iringa na nafikiri Mbeya iko karibu bei hiyo hiyo. *CAN* imepata ruzuku shilingi 500/= *anyway* orodha yenyewe ni ndefu sana lakini imepata ruzuku kwa asilimia hiyo na bei ninazo hapa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tusipoteze wakati, baada ya kujibu swali hili tuonane, nimfafanulie. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ruzuku iliyotolewa imesaidia sana katika mwanzo wa kilimo, lakini hivi sasa tunavyozungumza Mkoa wa Rukwa mbolea ya *Urea* hakuna. Mkoa wa Mbeya mbolea ya *Urea* hakuna na Mkoa wa Ruvuma.

Je, Serikali inafanya mbinu gani kuhakikisha kwamba mbolea hii inafika katika kipindi cha wiki moja au wiki mbili kabla msimu wa mazao haujapita?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyotoa kwenye suala la msingi na pili naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi kabla ya kuja hapa nimeshuhulikia suala hilo na tunatarajia muda wowote sasa tani 600 za mbolea zitapelekwa Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili tatizo litakuwa limepungua na tumetoa maagizo kwamba mbolea ipelekwe mara moja. Isitoshe tunafanya mipango ili kupata tani 30,000 za mbolea aina ya *Urea* katika kipindi kifupi iwezekanavyo ili iwahi mazao mazuri sana yaliyoko shambani hivi sasa. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha yale yaliyobaki yatashughulikiwa kama inavyoelekezwa na kanuni zetu za Bunge. Tunaendelea, kabla ya kuendelea tuna matangazo ya vikao vya Kamati mbali mbali kwa leo. Ziko Kamati nyingi zimejipangia kufanya vikao kama ifuatavyo:-

*Kamati ya Ulinzi na Usalama, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jackson Makwetta. Anaomba Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wakutane mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika chumba namba 133 ghorofa ya kwanza.*

Kamati nyingine ni ya Uwekezaji na Bishara, Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shellukindo anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, kutakuwa na kikao mara baada ya kipindi cha maswali na majibu. Chumba cha Kamati namba 231 ghorofa ya pili.

Kamati ya tatu ni ya Fedha na Uchumi, Mwenyekiti wake anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa 5 asubuhi hii katika chumba namba 231. Kamati ya Fedha na Uchumi kikao saa 5.

Kamati ya Maendeleo na Jamii, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Haroub Masoud, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane chumba namba 432 ghorofa ya nne saa 5 asubuhi hii.

Kamati ya mwisho ni ya Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda. Anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakute mara tu baada ya kuahirisha Bunge asubuhi hii yaani kunako saa 7 huko, chumba namba 218 ghorofa ya pili mchana.

Hii si Kamati lakini Mheshimiwa Zahor khamis ambaye ni Katibu wa Umoja wa Bunge wa CCM wa Zanzibar, anaomba Wabunge hao wa CCM kutoka Zanzibar wakutane mara baada ya kuahirisha kikao saa 7 wakutane chumba namba 37 ghorofa ya kwanza.

Mwisho wa matangazo tunaendelea na *order paper* Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Kumi na Nne Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Mwaka, 2004**

**Muswada wa sheria inayoainisha Majukumu na Kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2005 *(The AttorneyGeneral (Discharge of Duties) Bill, 2005***

**Muswada wa Sheria inayoainisha Masuala ya Kiutawala na Kinidhamu ya Majaji Wasajili na Utaratibu wa Ajira, Utumishi na Nidhamu ya Mahakama *(The Judicial Service Bill, 2005***

**Muswada wa sheria ya Uchaguzi wa Mwaka 2005 *(The Electoral Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005***

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill 2005***

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uaanzishwaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika mashariki *(Agreement on the Establishment of the Inter-University Council of East Afrifa)*

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw'. Mbunge wa Babati Mashariki na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati hiyo, kwa ushirikiano na ushauri wao walioniwezesha kuboresha Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipovunjika mwaka 1977, asasi nyingi zilizokuwa ndani ya Jumuiya zilivunjika. Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki ni mojawapo ya asasi zilizonusurika.

Aidha katika kutathimini umuhimu wa ushirikiano wa nyanja mbali mbali za elimu ya juu na utafiti. Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuuu vitatu vya Serikali yaani (Dar es Salaam, Nairobi na Makerere) walisaini Mkataba wa Maelewano *Memorundum of Understanding November 1980,* ambao ndio umekuwa ukiongoza shughuli za Baraza za Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1999 uliposainiwa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki lilipewa umuhimu wa kuendelezwa ndani ya Jumuiya hiyo. Kifungu cha 102 na cha 103 katika Mkataba huo vinahimiza ushirikiano katika elimu na mafunzo na sayansi na teknolojia.

Aidha sehemu ya 16 ya Mkataba huo kifungu kidogo cha 2(f) ukurasa wa 73 kinasisitiza kufufua na kuendeleza majukumu ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika kuhuisha na kuimarisha Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki tayari mabadiliko makubwa yameonekana kwa kipindi cha kuanzia mwaka 1999 Mkataba wa Jumuiya ya Afrika uliposainiwa. Mabadiliko hayo ni:-

I. Taratibu za uongozi wa Baraza zimekuwa bayana na kuwepo mgawanyo wa nafasi za uongozi unaozingatia nchi wanachama na kipindi maalum cha kukaa katika uongozi kwa kupokezana.

II. Kamati mbali mbali za Baraza zimerekebishwa.

III. Vyuo Vikuu binafsi vimekubaliwa kuwa wanachama.

IV. Vyuo na asasi wanachama vinatozwa ada ya uanachama kati ya dola za Kimarekani 500 hadi 1,000 kwa mwaka.

V. Mashirika na *Commission* za Sayansi na Teknoloji zimeingizwa katika uanachama.

Mheshimiwa Spika, muelekeo huo thabiti wa Baraza umesababisha Mashirika ya Kiamataifa yaanze kutoa misaada katika mafunzo na *scholarship.* Mfano, Shirika la *Ford Foundation* ambalo kuanzia mwaka 2002 hutoa nafasi 27 kila mwaka. Yaani nafasi tisa kwa kila nchi Tanzania, Kenya na Uganda kusoma Shahada ya Uzamili mahali popote duniani.

Mheshimiwa Spika, asasi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaongozwa kwa kutumia itifaki yaani *protocols.* Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki bado linaongozwa na Mkataba wa maelewano wa mwaka 1980 ambao umekwishapitwa na wakati.

KWA KUWA Baraza la Vyuo Vikuu ni asasi iliyo ndani ya Jumuiya inastahili kuongozwa na itifaki.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mawasiliano na wadau wa ndani ambao kwa kupitia mikutano mbali mbali waliichambua, kujadili na kuchangia katika kurekebisha itifaki hii. Wadau hao ni pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Wizara ya Elimu na Utamaduni, Wizara ya Elimu Utamaduni na Michezo Zanzibar. Vyuo Vikuu vya Umma na vyuo Vikuu vya binafsi, Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu, na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Vile vile rasima ya itifaki ilipitiwa na Kamati za *Senate* katika Vyuo Vikuu vyote vya Umma na Binafsi ndani ya nchi wanachama na kuafikiwa. Aidha ilipitiwa pia na Wizara ambazo ni wadau wa elimu ya juu katika Jumuiya. Kamati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Sekta ya elimu Wanasheria Wakuu wa Nchi Wanachama, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimaye kusainiwa na Mawaziri wanaohusika na Elimu ya Juu mwezi Novemba mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa Azimio la itifaki ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 sura ya 8 kifungu cha 8.2 kipengele cha 8.2.1 ukurasa wa 26, kinachosisitiza Serikali kuboresha na kuimarisha mahusiano na mashirikiano baina ya asasi za ndani na nje ya Nchi.Katika kutekeleza itifaki hii vyanzo vikubwa vya raslimali vitakuwa ruzuku kupitia bajeti za Serikali za nchi wanachama. Kila nchi inatakiwa kuchangia kwa kiwango sawa cha Dola za Kimarekani 295,937. Aidha kuna michango ya Vyuo Vikuu na asasi wanachama na misaada kutoka kwa wafadhili. Aidha napenda kutoa maelezao kwa ufupi

kuhusu manufaa ya Kuridhia Azimio la Itifaki ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

* Kuimarishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa katika elimu ya juu.

* Kuinua viwango vya ushindani vya Vyuo Vikuu katika nchi wanachama.

* Kuwezesha kubadilishana matokeo ya utafiti na uzoefu katika taaluma na utafiti.

* Kuimarisha taratibu za ulinganisho wa mitaala, mitihani, utambulisho wa vyeti na ithibati.

* Kuimarisha utaratibu wa kubadilishana wanafunzi, wanataaluma na watafiti miongoni mwa nchi wanachama.

* Tanzania itanufaika na *program* mbali mbali zinazotolewa na wafadhili na Mashirika ya Kimataifa kupitia Baraza la Vyuo Vikuu cha Afrika Mashariki.

Itifaki ya Baraza la Vyuo Vikuu itaanza kutumika baada ya kuridhiwa na nchi zote wanachama, na hati za ridhaa kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kusoma Azimio lenyewe yaani *"Protocol on the Establishment of the Inter- University Council for East Africa"*.

KWA KUWA Tanzania ni moja ya Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambazo zinazoshirikiana katika masuala ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii:

NA KWA KUWA kuanzia mwaka 1947 mpaka mwaka 1977 ushirikiano wa kiutamaduni na nyanja zingine viliendeshwa kwa maagizo yaliyotolewa na *"East Africa High Commission"* na baadaye kupitia mkataba wa ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967 - 1977:

NA KWA KUWA wakati wa ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kamati ya Vyuo Vikuu vya Afrika ilikuwa mojawapo ya asasi zilizotoa huduma za elimu ya juu:

NA KWA KUWA hata baada ya kuvunjika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, Vyuo Vikuu kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya Umoja wa Afrika viliamua na kuendelea kushirikiana katika nyanja mbali mbali za utafiti na elimu ya ju:

NA KWA KUWA kuanzia mwaka 1980 Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashiriki vinatoa huduma zake kwa misingi ya taratibu za Mkataba wa Maelewano yaani *(Memorandum of Understanding):*

NA KWA KUWA kwa mkataba wa mwaka 1999 wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki litatambuliwa kama asasi iliyonusurika kuvunjika katika Jumuiya hiyo:

NA KWA KUWA viongozi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamekubali kuhuisha rasmi Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki na kuunda itifaki itakayoongoza Baraza hilo:

KWA HIYO BASI kwa kuzingatia umuhimu huo na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania katika mkutano wake wa 18, sasa linaazimia kuridhia itifaki ya kuanzishwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki yaani *"Protocol on the Establishment of the Inter-University Council for East Africa."*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kabla hatujaendelea niseme tu kwamba mpaka sasa nina ombi la mchangiaji mmoja tu, kwenye Azimio hili Mheshimiwa Prof. Juma Mikidadi kama kuna mwingine ana nia ya kuchangia naomba alete karatasi. Sasa kwa utaratibu wetu namwita Mwenyekiti wa Kamati uliyopitia Azimio hili ili atoe taarifa ya Kamati.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitoe shukrani zangu kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii mlioipa jukumu la kufikiria Azimio la Bunge kuridhia itifaki ya kuanzishwa baraza la Vyuo Vikuu Afrika Mashariki. Kwa nafasi hii hii naomba kukutakia wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote heri, baraka na afya njema kwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipata maelezo fasaha ya Mheshimiwa Waziri wa Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu kuhusiana na umuhimu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuridhia itifaki ya baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki na kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ikizingatia kuwa Tanzania ni mwanachama wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinashirikiana katika masuala ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii na ukweli kuwa mara baada ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvunjika rasmi mwaka 1977. Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki ambalo lilikuwa limeundwa chini ya Mkataba uliyovunjwa liliona umuhimu wa kuendelea kushirikiana kwa kuweka taratibu za mkataba wa maelewano yaani *Memorandum of Understanding of the inter-university council of East Africa* mwaka 1980, ambao

uliwezesha Vyuo Vikuu vya nchi za Afrika Mashariki kuendelea kushirikiana katika nyanja za elimu, utafiti na mafunzo ambao ndiyo unatumika hadi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, umoja huu wa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki unatarajiwa kushirikisha Vyuo Vikuu vya nchi nyingine zilizo mashariki mwa Afrika kama vile Burundi, Djibouti, Eritrea, Ethiopia, Rwanda, Somalia na Sudan. Hivyo kamati yangu inatoa pongezi kwa uongozi wa Vyuo Vikuu vitatu vya Dar es Salaam, Makerere na Nairobi kwa kuanzisha na kuendeleza mahusiano hayo hadi itifaki hii kutungwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaunga mkono hoja hii kwa kuzingatia kuwa kuridhiwa kwa itifaki hii, Taifa letu litaendelea kunufaika katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa katika nyanja za elimu ya juu, mafunzo na utafiti. Kuinua viwango vya ushindani wa Vyuo Vikuu katika nchi wanachama, kuwezesha kubadilishana matokeo ya utafiti na uzoefu katika taaluma na utafiti, kuimarisha taratibu za ulinganisho wa mitaala, mitihani, utambulisho wa vyeti na ithibati na kuimarisha utaratibu wa kubadilishana wanafunzi, wanataaluma na watafiti miongoni mwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, vile vile Tanzania itanufaika na program mbalimbali zinazotolewa na wafadhili na mashirika ya kimataifa kupitia Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati yangu ilizingatia kuwa kuridhiwa kwa itifaki hii ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya taifa ya elimu ya juu kwa mwaka 1999, inayosisitiza Serikali kuboresha na kuimarisha mahusiano na ushirikiano baina ya asasi za ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu Kamati yangu inaunga mkono hoja ya Serikali kuomba Bunge lako Tukufu kuridhia itifaki ya kuanziwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huo wa kuridhia itifaki hii kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo:

1. Kutokana na umuhimu na faida za taifa letu kuwa mwanachama wa Baraza hili hasa katika taaluma na utafiti katika Elimu ya Juu. Kamati inaona ni vyema Vyuo Vikuu vyote vya Tanzania vya Serikali na vya binafsi kuwa wanachama wa Baraza hili la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kwa nia ya kubadilishana mitaala, wanataaluma na wanafunzi.
2. Vile vile kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Wizara ya Sayansi Teknolojia na Elimu ya Juu iandae mpango wa kuelimisha Vyuo Vikuu vyote nchini kuhusu umuhimu wa kuwa mwanachama wa Baraza hili.

Mheshimiwa Spika, mwisho kamati inaipongeza Serikali ya Tanzania kwa juhudi zake za kuchangia Baraza hili kikamilifu. Kwani Kamati imeona kuwa tangu Baraza lianzishwe kwa Mkataba wa maelewano yaani memorandum of understanding mpaka

sasa Serikali ya Tanzania imekuwa ikichangia kikamilifu. Huu ni ushahidi kuwa Serikali ya Tanzania imeonyesha uadilifu, uaminifu na uwajibikaji mbele ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tunashauri Serikali iendelee na uadilifu huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya kwa niaba ya Kamati ya Huduma za Jamii naunga mkono hoja ya kuridhia itifaki ya kuanzishwa kwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na taadhima, naomba nichukue nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kwa mujibu wa kifungu cha 43 kifungu kidogo cha 5b na 81 kifungu kidogo cha kwanza toleo la 2004. Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kabisa kwa niaba ya kambi ya upinzani Bungeni kuunga mkono Azimio hili la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Naunga mkona Azimio hili kwa sababu ya kuzingatia yafuatayo:-

(1) Historia ya ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki kuanzia mwaka wa 47 hadi 77.

(2) Kwa kuzingatia mkataba wa 1999 wa kuanzisha upya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(3) Kwa kuzingatia historia ya ushirikiano wa Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kwa kuzingatia Mkataba wao wa maelewano yaani *Memorandum of Understanding* ya mwaka 1980 na kama ulivyorekebishwa mnamo mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono Azimio hili Kambi ya Upinzani inaomba kuishauri Serikali kuchukua hatua zifuatavyo, ili Tanzania iweze kurekebisha hali na mazingira ya ufundishaji katika Vyuo Vikuu vya Tanzania hasa vile vya Umma ili kuleta ulinganifu kati yake na nchi zingine za Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mambo yanayohitaji marekebisho ni kama yafuatayo:-

* Umri wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.
* Idadi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.
* Marupurupu na mishahara ya waalimu wa Vyuo Vikuu.
* Miundombinu hasa madarasa, vyumba vya semina, maktaba na mabweni na *hostel* za wanafunzi katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia mnamo Julai mwaka 2004, katika kitabu kiitwacho *Some Basic Statistics*

*on High Learning Institution in Tanzania 1999/2000.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mathalani kilikuwa na idadi ya wanafunzi 6,739. Wakati huo huo kilikuwa na Wahadhiri 539, mnamo mwaka 2002/2003 wanafunzi walikuwa 10,148 na Wahadhiri walikuwa 545, na kwamba mwaka 2003/2004 wanafunzi walikuwa 10,549 na Wahadhiri walikuwa 549 ikiwa na maana kuwa ongezeko la idadi ya wanafunzi karibu 4,000 kulikuwa na ongezeko la walimu au Wahadhiri kumi tu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania mnamo mwaka 2001/2002, wanafunzi walikuwa 4,347 na Wahadhiri walikuwa 56 tu. Mwaka 2002/2003 wanafunzi walikuwa 5,683 na walimu walipungua na kuwa 47 tu. Mwaka 2003/2004 wanafunzi walikuwa 10,313 na walimu walikuwa 79 tu, kwa maana ya wastani wa wanafunzi 131 kwa mwalimu mmoja. Ni katika mazingira haya ambako hoja inajengwa kuwa kutokana na ongezeko la wanafunzi wengi na walimu kuwa wachache ni dhahiri kazi zinaongezeka sana kwa walimu wa Vyuo vyetu Vikuu. Hivyo kupelekea haja ya kuongezewa walimu marupurupu na mishahara yao. Pamoja na kuwa mishahara ya watumishi wote wa Tanzania haitoshi, lakini haiingii akilini kwa *Professor* wa shahada ya uhasibu na baadaye mwanafunzi wake akaajiriwa katika Idara ya Kodi na Mapato na mshahara wake ukawa mathalani shilingi 2,000,000. Hirari mshahara wa mwalimu wake ukiwa shilingi 500,000. Ni kutokana na kukatishwa kwa Waziri wa Vyuo Vikuu vyetu wanaacha kazi hapa nchini na kwenda nchi za nje au mashirika mengine ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa mwaka 1999 hadi 2000 idadi ya Wahadhiri wenye shahada ya Uzamini walikuwa 176, na mwaka 2003/2004 walipungua hadi 110 pungufu ya asilimia 66, na wale wenye shahada ya falsafa ya Udaktari wa mwaka 1999/2000 walikuwa 394, na mwaka 2003/2004 walikuwa 439. Wakati huo huo hakukuwa na walimu wenye shahada ya kwanza kwa maana ya wale *Tutorial Assistances* kutoka mwaka 2001/2002 hadi 2003/2004. Ni kutokana na taarifa hizi kuwa walimu wengi wanastaafu mapema na mara tu baada ya kupata udaktari wa falsafa na u-*professor* na hivyo kustaafu kabla ya kutumia ujuzi wao kwa manufaa ya wanafunzi wa Kitanzania. Vile vile ni kutokana na mtizamo wa Serikali wa kuongeza miaka ya kustaafu kwa Majaji wa Mahakama ya Rufaa Tanzania, tungependa mtizamo huo utumike kuangalia upya umri wa kustaafu wa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa ushauri kwa Serikali kuwa wakati sasa umefika wa kuboresha miundombinu katika Vyuo vyetu Vikuu, kama vile ujenzi wa madarasa, vyumba vya semina na mihadhara, maabara, mabweni ya wanafunzi na kadhalika. Kwa mfano katika mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Utakuta chumba kilichopangiwa kulala wanafunzi wawili wanalala wanafunzi sita, na hii sio shitaka kwamba wafukuzwe humo bali kwamba mabweni yaongezwe.

*Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni katika Makao Makuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Kanda ya Dar es Salaam, Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu inatia aibu. Pamoja na yeye kutokuwa na gari la kazi. Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2004/2003 nilitoa takwimu zilizoonyesha kuwa ifikapo mwaka 2015. Tanzania itakuwa na jumla ya wanafunzi zaidi ya 125,000 wanaopaswa kujiunga na Vyuo Vikuu vya Umma.*

Sasa ni kutokana na kuliona hilo naikumbusha Serikali mapema juu ya kuandaa mazingira ya sasa ya kuongeza idadi ya Wahadhiri wa Vyuo Vikuu mapema, kuangalia sheria inayohusu umri wao wa kustaafu, kuwaongezea marupurupu yao ili waweze kuendelea na kazi, kuongeza miundo mbinu kama nilivyotaja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, najua kuwa agenda ya leo ilihusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Baraza ya Vyuo Vikuu vya Afrika ya Mashariki, lakini ni kwa kuzingatia ukweli kuwa sisi tunao wahitimu wachache kutokana na wanafunzi wachache waliopo katika Vyuo vyetu Vikuu. Vinginevyo kuendelea kujivunia mafanikio ya MMEM na kukazania *Education For All (EFA)* Elimu kwa Wote kwa maana ya Elimu ya Msingi tutakuja kukosa mwelekeo hapo baadaye kwani hakuna nchi hapa duniani iliwahi kuendelea kiviwanda, kiuchumi na kiteknolojia kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya watu wake walikuwa wamepata Elimu ya Msingi au Sekondari.

Katika hili, Tanzania ni ushahidi tosha kwamba hadi miaka ya 1980 Tanzania iliongoza Barani Afrika kwa kuwa na wananchi wake zaidi ya asilimia 80 waliojua kusoma na kuandika kutokana na mpango wa *UPE* na Elimu ya Watu Wazima. Hivyo badala ya kusherehekea na kuselebuka kuhusu mafanikio ya MMEM, Taifa lingekuwa linakosa usingizi kwa kutafuta mbinu, mikakati na raslimali za kuinua na kuendeleza Elimu ya Juu, Sayansi , Teknolojia mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kwamba naunga mkono Azimio hili kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kama nilivyoeleza, nina msemaji mmoja tu katika hoja hii, sasa nampa nafasi Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mheshimiwa Mtoa hoja ujiandae kuhitimisha hoja yako.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wabunge wote, awali ya yote nakupeni heri ya mwaka mpya, nakutakieni fanaka mwaka huu uwe wa baraka na mwaka wa heri na Uchaguzi utakaofuata, Wabunge wote warudi kama walivyo Mungu akipenda. *Inshallah. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa kuwasilisha Azimio hili kwetu kwa ufasaha pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa kulichambua Azimio hili na kulifikisha kwetu. Nalipongeza Baraza kwani halikuweza kufa pale Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipokufa 1977. Huu ni ushahidi tosha wa kuonyesha kwamba Baraza linaweza kufanya vizuri zaidi ikiwa litaweza kuboresha mambo yale ambayo yanaonekana yana hitilafu hapa na pale hasa hasa katika sehemu zile ambazo nchi zinahitaji msaada mkubwa kwa mfano Tanzania. Kwa nini nasema hivyo?

Ni kwa sababu idadi yetu ya Wataalamu katika Tanzania ukilinganisha na nchi zetu jirani za Afrika Mashariki mathalan Kenya na Uganda, hapa kwetu inaweza kuwa idadi yetu ni ndogo zaidi hata ukichukua idadi ya wanafunzi wanaoingia au waliokuwa katika Vyuo Vikuu katika Tanzania ukilinganisha na Kenya na Uganda kwamba sisi tuko nyuma. Pengine sisi ndio ambao tulikuwa tuna haja kubwa zaidi ya kuliangalia Baraza hili jinsi gani tutaweza kufaidika kwa yale ambayo yatakayofanywa kwa ajili ya maendeleo ya taaluma katika nchi yetu.

Najua kwamba kuna juhudi kubwa zilizokuwa zinafanywa na Baraza hili ili kuweza kuoanisha mipango ya taaluma kati ya Tanzania, Kenya na Uganda na zile nchi jirani ambazo zinataka kujiunga na utaratibu huu au zimejiunga na utaratibu huu. Lakini kitu ambacho ninataka kukizungumza ni kimoja tu kwangu, bado maslahi ya Wahadhiri pamoja na Maprofesa hasa hasa katika Vyuo Vikuu vya Tanzania yako chini sana ukilinganisha na Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Kenya nafundisha Chuo Kikuu cha Nairobi. Ukilinganisha maslahi ya Waalimu katika Chuo Kikuu cha Nairobi au Vyuo Vikuu vya Kenya na vya Tanzania utaona kusema kweli Vyuo Vikuu vya Tanzania maslahi yake yako chini sana na wakati fulani tulikuwa tunashangaa sio kushangaa tu hasa tulikuwa tunahoji kwa nini Wahadhiri watoke au wakimbie kutoka Vyuo Vikuu vya Tanzania kuelekea Kenya au Uganda au kwenda Botswana? Mathalan ilikuwa ni kwa sababu maslahi yako chini.

Kwa hiyo, mimi nasema tutaridhia Azimio hili lakini Baraza liangalie uwiano wa jinsi Wahadhiri pamoja na Maprofesa wanavyolipwa hapa Tanzania ukilinganisha na Kenya na Uganda, kwa sababu kitu kitakachokuwa kinatuleta sisi katika hali mbaya zaidi pale ambapo tutaanzisha Shirikisho la Afrika Mashariki kuna *Fast Track* ya kuanzisha *East African Federation* ambayo *by the year 2010* jambo hilo linataka lifanyike, wakati ambapo ukiangalia sisi huku Tanzania ukilinganisha na Kenya na Uganda Tanzania bado iko chini jamani kitaaluma na kimaslahi. Sitaki kurudia aliyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu idadi ilivyo chini baina yetu Tanzania, Kenya na Uganda lakini kwa ujumla ni kwamba kuhusu maslahi kuna *drift of Professors and intellectuals* kutoka katika Vyuo Vikuu hivi kwenda *else where* ama *South Africa,* Botswana au Kenya na kwingine, sasa ili kuzuia hilo Baraza hili litakuwa na kazi ya kuoanisha haya maslahi kwanza kabla ya chochote.

Pili, mazingira ya wanafunzi pamoja na taaluma yenyewe bado Tanzania nadhani tuko nyuma. Sasa hivi katika *Secondary Schools* zilizoanzishwa na *International School* za wananchi wa Tanzania utaona Waalimu wengi au robo tatu au karibu wote wanatoka Kenya na Uganda jambo ambalo linasikitisha sana. Kwani hapa sisi Watanzania hatuna Walimu? Hatuna watu wa kufanya kazi hiyo mpaka iwe lazima tuwachukue kutoka Kenya! Sisemi kwamba hawa wasije hapa, lah! Sasa hivi tuna *East African Community* sawasawa, lakini tutakuja kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, *Free Movement of Services, Free Movement of Labour* hiyo inakuja kesho au keshokutwa. Lakini ninachosema, Tanzania bado tuna haja; tuna safari ndefu ya kuweza kufikia pale ambapo wenzetu wamefika na hili ni jambo la ndani sisi wenyewe tunaridhia kweli Mkataba wa

Kuanzisha Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki lakini sisi Tanzania bado tuna safari kubwa au ndefu ya kuweza kufikia pale wenzetu walipo.

Mheshimiwa Spika, sisemi kwamba elimu yetu ipo chini sana, la hasha; wala sisemi kwamba hatuna wataalamu hata kidogo; wapo lakini hatujawaangalia vya kutosha; hatujawaangalia ili kuboresha haya ambayo tunayafanya; tunafanya juhudi kubwa nakubali ingawa Msemaji wa Upinzani anazungumza juu ya EFA. Tusijivunie hiyo wala tusijivunie kuhusu MMEM na sasa hivi MMES. Tumefanya kazi nzuri lakini bado tuna kazi nyingine kubwa zaidi ya kuboresha hawa watu wenyewe wanaoendesha *program* hizo za taaluma ikiwa ni MMEM au MMES au katika Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka nishauri kwamba hili Baraza baada ya sisi kupitisha hapa lifanye kazi ya kuoanisha sasa mazingira ya taaluma kwa nchi zote tatu na zile ambazo zote zitakazokuwa zimejiunga na Baraza hili ili kuona tunakwenda pamoja na siyo wengine wanaachwa nyuma kimaslahi na wengine wako mbele. Lazima pawe na uwiano.

Jambo la pili ni juu ya ukuzaji wa mitaala. Mimi nafikiri suala la ukuzaji wa mitaala, *Develoment of Curriculum Studies* ni lazima lifanywe pia kwa mashirikiano ya nchi zote ambazo zinachangia katika Baraza hili. Maana yake ni nini? Yaani kuwe na utaratibu wa kuweza kukaa na kuona kwamba mitaala yetu inalingana kwa sababu tutakuwa na *platform* moja au tuna *platform* moja *of course* tunaanza hiyo baada ya kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki tutakuwa na *platform* moja ya wataalamu, sasa isije kuwa kwamba wataalamu wa nchi moja au wa mahali pamoja wakawa juu kuliko wataalamu wa sehemu nyingine, wakachukua nafasi hata zile za wale kule walikokuwa. Kwa hiyo, hilo litakuwa ni jambo ambalo litatusikitisha na siyo kutusikitisha tu, bali watu wetu watakuwa nyuma katika kupiga hatua kimaendeleo. Hivyo basi, mimi ningeshauri katika ukuzaji wa mitaala pawe na uwiano kuwe na jambo ambalo litaweza kuweka pamoja mitaala hii iwe katika utaratibu mmoja.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo wamelisema wenzangu, nataka kulititilia mkazo tu na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Naibu Waziri wamelitilia mkazo ni juu ya faida ambazo Tanzania tumekuwa tukizipata, si tu za kubadilishana wanafunzi na zile *scholarship* 27, sisi tisa, Kenya tisa na Uganda tisa bali itabidi tuongeze sasa idadi ya wanataaluma. Kuongeza idadi ya wanataaluma maana yake nini? Maana yake ni kwamba tuongeze ufanisi wa kuweza kupata wanataaluma zaidi katika kila nyanja na hilo linawezekana tu ikiwa Serikali itatilia mkazo kutoa ruzuku zaidi kwa hawa wanataaluma kufanya *research* na kuendeleza vitu ambavyo vitaweza kuwafanya wawe *competent* katika taaluma zao. Kwa hiyo, suala la *research* na suala la taaluma kuongeza kuhusu kiwango cha idadi ya wanataaluma ni jambo ambalo lazima tulititilie mkazo na Serikali iwaenzi wale ambao wanafanya kazi hizo hasa wale wanataaluma waliokuwa tayari katika *field* kwa muda mrefu watambue taaluma zao.

Nafurahi kwamba wanataaluma watatu, wanne hivi wamepewa tuzo na mmoja ni Profesa Mhalu wa Chuo Kikuu Muhimbili na wengine wawili mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwingine kutoka katika Vyuo vingine. Ninafurahi

wameanza hawa watatu lakini isiishie hapo tu. Wataalam wengi zaidi waweze kuenziwa ili waongeze kasi ya kuweza kufanya hii *cadre* ya wataalamu iwe kubwa zaidi na iendelee mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kwa hayo machache naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nampa nafasi Mheshimiwa Mtoa hoja ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ningependa niwatambue wale wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza. Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mbunge wa Babati Mashariki; Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi, Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Mbunge wa Kyerwa na mwisho ni Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mbunge wa Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru kwa dhati wote waliochangia na napenda niseme kwamba ushauri na maoni waliyoyatoa tutayazingatia katika kuboresha utendaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Kamati yake kwa ujumla kwa kuvishauri vyuo vikuu vyote nchini ambavyo havijaomba uanachama vifanye hivyo kwa manufaa yao, kwa manufaa ya elimu ya juu nchini na kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

Aidha, Wizara yangu itazingatia mpango wa kuelimisha Vyuo Vikuu vyote nchini ambavyo havijapata ithibati kufuata hatua zote ili ziweze hatimaye kuomba uanachama wa *Inter-University Council for East Africa* kwani hiki ni kigezo muhimu cha kujiunga na Baraza.

Mheshimiwa Spika, tunapokea pongezi za Kamati ya Huduma za Jamii kwa kuahidi kuchangia kiwango kilichowekwa kikamilifu na Baraza la *Inter-University Council for East Africa* kwa vile linao umuhimu wa manufaa kwa Taifa letu. Mpaka sasa Tanzania imekwisha changia michango yake yote kikamilifu katika Baraza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia vile vile kumshukuru Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa mchango wake ambao kwa hakika utasaidia kwa kiwango kikubwa kuboresha utendaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. Aidha, namshukuru yeye pamoja na Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono hoja hii. Mheshimiwa Mutungirehi alitoa hoja ya kuboresha mazingira ya ufundishaji wa vyuo vikuu vya Tanzania. Tumezingatia maoni na ushauri ili kuboresha

na kuviwezesha viwango vya taaluma vilivyotolewa na Vyuo vyetu Vikuu na ametoa pia hoja ya kuongeza idadi ya Wahadhiri.

Mheshimiwa Spika, hili tatizo linafahamika na linafanyiwa kazi katika Vyuo Vikuu kwa kuwapatia mafunzo Walimu wengi zaidi na kutangaza kazi za Wahadhiri katika magazeti yetu. Vile vile amezungumzia kuhusu kuboresha miundo mbinu. Hili pia limefanyiwa kazi ili kuboresha miundombinu na ni mojawapo ya mikakati inayoshughulikiwa. Aidha, Mfuko wa Elimu Tanzania unakopesha vyuo vikuu kwa ajili ya kuboresha miundombinu. Naomba sasa nijibu hoja za Mheshimiwa Profesa Juma Mikidadi, Mbunge wa Kibiti. Amezungumzia kuhusu maslahi ya Wahadhiri kwamba yaboreshwe. Ameeleza kwamba Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Tanzania maslahi yao ni madogo ukilinganisha na Wahadhiri wa nchi jirani mfano za Kenya na Uganda. Hili linafahamika na linafanyiwa kazi kwa pamoja na wafanyakazi wengine. Hili linafanyiwa kazi na Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuzaji wa mitaala, pia Mheshimiwa Mikidadi ameshauri kwamba kuwe na uwiano. Napenda kujibu kwamba, moja ya shughuli ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki ni kuweka uwiano katika mitaala na Vyuo Vikuu vyote vilitakiwa kutuma mitaala kwenye *Secretariat* ya Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika na Vyuo Vikuu vyote vya Tanzania vilikwishafanya hivyo tangu mwaka jana.

Mhehimiwa Spika, Mheshimiwa Mikidadi vile vile ameongelea kuhusu mazingira ya wafanyakazi kuwa yaboreshwe. Hivi sasa Serikali imekwishaanza kujenga vyumba vya mihadhara, nyumba za Walimu na kama nilivyosema kwa kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania, Vyuo vinakopeshwa ili viweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa mara nyingine ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote watatu ambao wametoa michango yao na michango hiyo itasaidia sana katika kuboresha utendaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Africa Mashariki liliridhiwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kueleza kwamba, kuna Maazimio mawili kwenye *Order Paper* lakini la pili tulipatana na Mwenyekiti wa Kamati inayohusika kwamba walikuwa wana kazi ndogo ya kumalizia kulifikiria hili Azimio na wangependa wakutane asubuhi ya leo. Alinihakikishia kwamba ni kazi ndogo tu watamaliza asubuhi ya leo.

Kwa hiyo, tukaliweka Azimio hili kwenye *Order Paper* kwa madhumuni kwamba litawasilishwa saa za mchana, Kipindi cha mchana cha Kikao cha Bunge. Kutokana na makubaliano hayo, sasa hivi Kamati inaendelea na shughuli hizo. *(Makofi)*

Sasa kwa ajili ya makubaliano hayo, napenda kusema kwamba shughuli zilizopangwa kwa Kikao cha asubuhi sasa zimekamika. Kwa hiyo, sasa nitasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 5.22 Asubuhi Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia kiti)*

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Tanzania Kujiunga na Utaratibu wa *(Africa Peer Review Mechanism (APRM)"* Chini ya Mpango na Ushirikiano Mpya ili kuleta Maendeleo Barani Afrika *(New Partnership for Africa's Development (NEPAD)***

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa vile hiki ni kikao chetu cha kwanza cha Bunge kwa mwaka 2005, nianze kukutakia wewe wenyewe na Wabunge wenzangu wote kheri ya mwaka mpya 2005. *(Makofi)*

Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Njelu Kasaka Mbunge wa Lupa, kwa uchambuzi na michango yao ambao wamekwishatoa kuhusu hoja hii. Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi walishiriki katika Semina iliyofanyika tarehe 26 Januari, 2005 Dar es Salaam na leo asubuhi wamepitia Azimio ninaloliwasilisha leo katika Bunge hili Tukufu. Waheshimiwa Wabunge wametoa michango mingi ambayo itazingatiwa wakati wa utekelezaji. Pamoja na mambo mengine michango yao imesisitiza umuhimu wa *Africa Peer Review Mechanism* kwa maendeleo ya Afrika, umuhimu wa kuelimisha wananchi kwa jumla na umuhimu wa kushirikisha wadau wote katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 90 uchumi wa sehemu nyingi duniani isipokuwa wa Bara la Afrika uliimarika. Uchumi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikua kwa wastani wa asilimia 2 wakati idadi ya watu iliongezeka kwa asilimia 2.8, pamoja na kwamba mwenendo ulianza kuwa na ahueni kuanzia miaka ya 95 kufuatia marekebisho ya sera za uchumi katika nchi nyingi za Afrika. Kwa sababu hii jukumu la maendeleo Barani Afrika bado ni kubwa kwani Bara hili ndilo lenye watu wengi maskini wenye kipato kidogo. Kiwango kikubwa cha ujinga na wastani mdogo wa miaka ya kuishi. Zaidi ya asilimia 40 ya watu wa Afrika huishi katika umaskini uliokithiri wakati ambapo janga la UKIMWI linazidisha matatizo kwa Afrika. Mfumo wa uchumi Barani Afrika unakabiliwa na matatizo mengi hasa kwa kuwa nchi za Afrika hutegemea

uzalishaji wa mazao machache asilia ambayo bei zake katika soko la Kimataifa hushuka au kuyumba mara kwa mara.

Nchi hizi zina viwango vidogo sana vya uwekaji akiba na uwekezaji raslimali na Afrika imegawanyika katika nchi nyingi zenye masoko madogo yasiyoweza kuvutia shughuli nyingi za kiuchumi. Aidha, Afrika inakabiliwa na migogoro mingi ambayo hurudisha nyuma maendeleo ya watu wake na kuifanya isiwe kivutio kizuri kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupambana na umaskini Barani Afrika katika Kikao cha Viongozi wa Nchi za Afrika kilichofanyika mwaka 1998 huko Sirte, Libya Rais Thabo Mbeki wa Afrika ya Kusini, Rais Olusegun Obasanjo wa Nigeria na Rais Abdalaziz Bouteflika wa Algeria walipewa jukumu la kuandaa Mpango wa Maendeleo kwa ajili ya Afrika na kuongoza juhudi za kuwasiliana na kundi la nchi tajiri duniani G8 ili kusukuma mbele hoja ya Afrika kutaka kufutiwa madeni. Kwa wakati huo Rais Bouteflika alikuwa Mwenyekiti wa *AU,* Rais Mbeki Mwenyekiti wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote na Rais Obasanjo Mwenyekiti wa *G 77.* Viongozi hawa kwa kushirikiana na Rais Hussein Mubarak wa Misri na viongozi wengine wa Afrika waliandaa rasimu ya mpango iliyojulikana kama *the Millennium Partnership for the African Recovery Programme - MAP.* Wakati maandalizi ya MAP yakiendelea Rais Abdoulaye Wade wa Senegal alifanya juhudi kutayarisha Mpango wa Kukabiliana na Matatizo ya Uchumi Yanayoikabili Afrika. Yeye aliandaa rasimu ya mpango iliyojulikana kama *OMEGA Plan of Action for Africa - OMEGA.* Katika Mkutano wa Viongozi wa Afrika uliofanyika huko Lusaka Zambia mnamo Julai, 2001 MAP na *OMEGA* ziliunganishwa na kuzaliwa *New African Initiative.* Katika Kikao cha Kamati ya Kusimamia utekelezaji wa Mpango huu kilichofanyika Abuja tarehe 23 2001, jina lilibadilishwa na kuwa *New Partnership for Africa's Development (NEPAD)* ili kusisitiza umuhimu wa ushirikiano ndani ya kila nchi Afrika na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NEPAD* ni tamko la pamoja la Viongozi wa Afrika la kuongoza juhudi za kuondoa umaskini katika nchi zao na kwa Afrika yote na wakati huo huo kuifanya Afrika ichukue nafasi yake katika masuala ya uchumi na siasa Kimataifa. Viongozi wa Afrika waliona huu ndiyo wakati muafaka wa programu hii kwa kuzingatia rasilimali nyingi zilizopo Afrika, kupanuka kwa demokrasia Barani Afrika, kupanuka kwa utandawazi na kuwepo kwa dhamira ya Kimataifa ya kupiga vita umaskini na kupunguza mzigo wa madeni kwa Afrika. Lengo la *NEPAD* ni kufikia kiwango cha ukuaji uchumi cha wastani wa asilimia 7 na kufuta umaskini kwa nusu ifikapo mwaka 2015. Aidha, lengo pia ni kufikia viwango vya maendeleo vilivyowekwa Kimataifa *Millennium Development Goals 2015* kuhusiana na hali ya umaskini, elimu ya msingi, tofauti za kijinsia, afya na mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili *NEPAD* iweze kufanikiwa mambo manne yamepewe kipaumbele.

Kwanza, mambo ya lazima kwa maendeleo endelevu ya Afrika. Ili kuwa na viwango vizuri vya maendeleo endelevu Barani Afrika *NEPAD* imebaini kwamba ni

lazima kwanza pawepo na hali ya amani, usalama, demokrasia na utawala bora, kisiasa na kiuchumi. Kwa kuzingatia umuhimu wa kipengele hiki utaratibu wa *African Peer Review Mechanism* umeanzishwa ili kupima utekelezaji wa *NEPAD* kwa kila nchi shiriki ya *NEPAD* kwani uzoefu umeonyesha kwamba Afrika imepoteza rasilimali na fursa nyingi kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe, ukosefu wa utawala bora na matumizi ya sera dhaifu za uchumi katika nchi nyingi.

Pili, vipaumbele vya kisekta. *NEPAD* imeweka kipaumbele katika kwanza, miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, bandari, reli, njia za majini, mawasiliano, nishati na maji. Lengo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma na kupunguza gharama uzalishaji na utoaji huduma, kuimarisha ushirikiano, kuendeleza biashara kikanda na kuendeleza ushiriki wa sekta binafsi.

Pili, maendeleo ya nguvu kazi hasa kuhusiana na elimu ya msingi na Sekondari, Elimu ya Vyuo Vikuu na kujenga mazingira yatakayovutia wataalam wa Afrika walio nje kurudi na kubaki Afrika. Lengo pia ni kuimarisha huduma za Afya hasa kwa kupiga vita magonjwa yanayoambukizwa kama UKIMWI, Malaria na kuboresha lishe. *(Makofi)*

*NEPAD* itaelekeza nguvu katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo la kilimo kutegemea mno mvua, kuimarisha huduma za utafiti na ugani na kuelekeza rasilimali zaidi za umma na sekta kwenye kilimo binafsi.

Sekta nyingine ni mazingira, sayansi, teknolojia, biashara na utamaduni.

Tatu, Raslimali za utekelezaji wa *NEPAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia lengo la ukuaji wa uchumi kwa asilimia 7 kwa mwaka na kufuta umaskini kwa nusu ifikapo mwaka 2015 *NEPAD* inakadiria kuwepo kwa pengo la rasilimali sawa na asilimia 12 ya pato la Taifa au dollar za Kimarekani bilioni 64. Katika kipindi cha muda mfupi inatarajiwa kuwa pengo hili litafidiwa na kuongeza mapato ya ndani, misamaha ya madeni na misaada.

Kipindi hiki kitatumika kujenga uwezo na kuweka mazingira yanayochochea maendeleo endelevu yenye upeo wa muda mrefu. Kwa upeo wa muda mrefu tegemeo kubwa katika kuendeleza Afrika lipo kwenye uwekezaji raslimali kutoka ndani na nje na kwenye rasilimali zinazotokana na biashara ya bidhaa zetu. Afrika inazo rasilimali na fursa nyingi za kuendelezwa kwa kutumia uwekezaji wa ndani na nje; na kwa kuendeleza biashara kati ya nchi za Afrika na kati ya Afrika na Mabara mengine. Njia hii ndiyo itawezesha Afrika kuendelea bila kuzidi kuwa tegemezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kuhusu Ushirikiano wa Kimatatifa. Mafanikio ya *NEPAD* yatategemea pia kuwepo kwa ushirikiano mzuri kati ya Afrika na Mataifa mengine. Inategemewa kwamba nchi zilizoendelea zitaunga mkono kwa dhati juhudi za nchi shiriki za *NEPAD* hasa katika kuzima na kuzuia migogoro, kutoa unafuu wa madeni kwa nchi zinazoendelea zenye kipato cha chini na kuongeza misaada hadi kufikia

viwango vinavyokubaliwa Kimataifa. Viwango hivyo ni kwa nchi zilizoendelea kutoa kiasi kisichopungua asilimia 0.7 ya pato la Taifa *GNP* kama msaada kwa nchi zinazoendelea. Nchi ambazo zimetimiza lengo hilo ni Denmark, Luxembourg, Netherlands, Norway na Sweden. Aidha, ili nchi maskini zaidi duniani zipewe kipaumbele katika misaada ya maendeleo. Lengo la pili la Kimataifa ni kwa kila nchi iliyoendelea kutoa misaada kiasi kisichopungua asilimia 0.2 ya pato la Taifa kwa nchi maskini zaidi duniani. Nchi zilizofikia lengo hilo ni Norway, Denmark, Luxembourg Netherlands, Sweden na Ireland.

Aidha, nchi zilizoendelea hutegemewa kuunga mkono juhudi za kufungua masoko yao kwa bidhaa za nchi za Afrika na kuwahamasisha wawekezaji Barani Afrika. Jumla ya nchi maskini zaidi duniani ni 50 na kati hizo 34 zipo katika Bara la Afrika. Mawasiliano yamekwishafanyika na kundi la nchi tajiri, Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia, *TICAD* na baadhi ya nchi moja moja. Kwa jumla Jumuiya ya Kimataifa imeonyesha kuunga mkono *NEPAD*, changamoto ipo katika kutekeleza utaratibu *APRM* kuandaa programu za utekelezaji kwa kushirikisha Jumuiya za Ushirikiano kama *SADC, EAC, COMESA* na kuhusisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kupima na kutathmini utekelezaji wa malengo na vigezo vya utawala bora na uendeshaji uchumi *African Peer Review Mechanism.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi katika utekelezaji wa *NEPAD.* Utaratibu wa kupima na kutathmini utekelezaji na mafanikio ya mpango umeanzishwa. Huu ni utaratibu rasmi wa kubainisha mafanikio na mapungufu ya utekelezaji katika kila nchi shiriki, kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuboresha utekelezaji na kubanana kwa nchi shiriki Peer Pressure ili kuhakikisha kila nchi inatoa kipaumbele kwa Maazimio ya *NEPAD.* Kubanana kutafanyika kwa kufanya uchambuzi wa kina, kutolewa kwa taarifa zenye mapendekezo rasmi, kufanya majadiliano ya taarifa hizo katika vikao rasmi vya Umoja wa Afrika na *NEPAD* kulinganisha utekelezaji kinchi na kujadili taarifa zitakazotolewa ndani ya nchi husika. Maeneo yatakayofanyika tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yatafanyiwa tathmini ni yale yaliyobainishwa kuwa ni muhimu na ya lazima kwa maendeleo endelevu ya Bara la Afrika. Maeneo hayo kwanza ni Utawala Bora. Baadhi ya vipengele vitakavyotathminiwa vinahusu hatua za kuzuia migogoro ya ndani na nje ya nchi, utawala wa sheria, uhuru wa kujiunga na kuanzisha vyama kisheria, nafasi na haki za kushiriki katika chaguzi uhuru za viongozi, utenganisho kwa mamlaka za mihimili mitatu ya Serikali, vita dhidi ya rushwa, haki za makundi yanayoweza kuathirika kirahisi katika jamii pamoja na haki za wanawake na watoto.

Pili, uendeshaji wa uchumi. Vipengele vitakavyotathminiwa ni vile ambavyo ni muhimu katika kuweka mazingira ya uchumi endelevu, kuchochea ufanisi wa uchumi soko, kuzuia utumiaji mbaya wa rasilimali na kuhamasisha uwekezaji. Vipengele vingine vinahusu sera za mapato na matumizi ya Serikali, usimamiaji wa deni la Taifa,

utawala bora katika uendeshaji wa Makampuni, *good cooperate governance,* vigezo vya Kimataifa vya uwekezaji na ukaguzi wa mahesabu na usimamizi wa mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, watakaofanya tathmini. Upimaji utafanywa na Kamati ya watu mashuhuri watakaochaguliwa na viongozi wa Afrika kwa kuzingatia uwezo wao kitaaluma, maadili yalithibitika na uwakilishi wa maeneo ya Afrika. Watu hawa watasaidiwa na Taasisi zenye ujuzi na uzoefu. Kamati iliyochaguliwa hivi sasa inaundwa na wafuatao:-

Kwanza, Madame Marie Angelique Savane wa Senegal, Kanda ya Magharibi ambaye ni Mwenyekiti, Balozi Bethuel Kiplagat wa Kenya, Kanda ya Mashariki na Makamu Mwenyekiti, Dr. Graca Machel Afrika Kusini, Kanda ya Kusini, Prof. Adebayo Adedeji, Nigeria, Kanda ya Magharibi na Dr. Dorothy Njeuma Cameroon Kanda ya Afrika ya Kati. Ili utaratibu huu uwe na matokeo yanayoaminika na kuheshimika ni lazima ufanyike kiutaalam. Aidha, ni lazima tathmini zisifanywe kwa lengo kuumbuana, kuchokozana au kwa sababu za kiuhasama kwani kufanikiwa kwa zoezi hili kunategemea sana kuaminiana kati ya nchi inayotathminiwa na wanaofanya tathmini na miongoni mwa nchi shiriki za *NEPAD.* Aina za tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo aina nne za tathmini chini ya *APRM* kama ifuatavyo:-

Kwanza, tathmini ya awali ya kupima na kufahamu hali ilivyo kwa nchi. Hii inafanyika mara tatu nchi inapojengwa na utaratibu huu.

Pili, tathmini itakayofanyika kila baada ya miaka miwili.

Tatu, tathmini itakayofanyika wakati wote nchi shiriki ya *NEPAD* inapoomba ifanyiwe kwa matakwa yake.

Nne, tathmini itakayofanyika pale dalili za matatizo makubwa ya kisiasa au kiuchumi zitakapojitokeza. Lengo ni kuweza kuiangalia nchi husika mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini zote zitafanywa kwa kushirikisha viongozi wa Serikali, Mabunge, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Kiserikali, wanataaluma, Jumuiya ya Wafanyakazi na kadhalika. Katika kutekeleza utaratibu *APRM* hapa nchini itakuwa muhimu kuweka mfumo usimamizi na ufuatiliaji ambao ni shirikishi. Mfumo huo utajumuisha wadau kutoka Serikalini, Bunge, Mahakama, Sekta Binafsi, Vyombo vya Habari, Jumuiya zisizo za Kiserikali, Wanawake na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya *APRM* itasaidia kuzifanya nchi shiriki za *NEPAD* kuheshimu makubaliano na vigezo vya utawala bora, kuendesha uchumi kwa kutumia sera nzuri ambazo hutoa fursa kwa sekta binafsi, kujenga uwezo wa kupenyeza bidhaa za nchi mbalimbali katika soko la kanda na la Kimataifa kwa ushindani na kuimarisha ushirikiano ulio endelevu.

Aidha, mpango utaiwezesha Afrika kutathmini na kupima utekelezaji wa mambo yake yenyewe pasipo kusubiri kupimwa na Asasi kutoka nje ya Bara la Afrika. Aidha, *APRM* unadhihirisha kuwa Afrika iko tayari kufanya mabadiliko ya kukabiliana na changamoto za maendeleo bila kusitasita. Hii itafanya wadau wa maendeleo ya Afrika kuwa na imani na uhakika na sera na sheria zinazotumika katika nchi mbalimbali za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi kwa upande wa Tanzania.Tanzania ipo katika hatua nzuri ya kushiriki katika mpango wa *NEPAD* kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hii ni kwa kuwa Tanzania imekuwa mstari wa mbele kufanya marekebisho ya mifumo yake ya utawala, siasa na uchumi. Aidha, Tanzania inatekeleza programu nyingi chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ambazo ushabihiana na lengo la *NEPAD.* Programu hizo zipo katika maeneo ya utawala bora, uendeshaji uchumi na mipango ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Kuhusu utawala bora kisiasa. Mikakati ambayo Tanzania imekuwa ikitekeleza ili kuimarisha utawala bora nchini ni pamoja uendeshaji chaguzi za Vyama Vingi, kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, Vita dhidi ya Rushwa, Programu ya kuboresha Utumishi wa Umma, Programu ya kuimarisha sekta ya sheria, programu ya kuboresha Serikali za Mitaa na uimarishaji wa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali.

Pili, uendeshaji uchumi. Katika suala la Utawala Bora wa Uchumi Serikali inaendeleza sera na hatua za kuleta utegemavu wa uchumi hasa kwa kudhibiti ongezeko la bei, kusimamia vizuri matumizi na mapato ya Serikali, kuimarisha usimamizi wa mabenki na vyombo vya fedha, kujenga mazingira yanayowezesha sekta binafsi kushiriki katika uchumi.

Mipango ya Maendeleo. Kuhusu hatua za kuleta maendeleo kwa wananchi Tanzania inatekeleza mpango wa kufuta umaskini ambao malengo yake ni kuinua ubora wa maisha ya Watanzania, kujenga uchumi imara wenye kuhimili ushindani na kuweka misingi imara ya uongozi bora na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeandaa programu zake na kuendelezwa chini ya mpango wa *NEPAD* na kuziwasilisha katika sekretarieti ya *NEPAD* ya Jumuiya za Kanda. Programu hizo ni zile zinazoimarisha ushirikiano kikanda, zinazochangia kuinua vipato na kufuta umaskini na zinazoendeleza amani na utulivu katika kanda yetu. Baadhi ya programu hizo ni pamoja na daraja la Umoja Ruvuma, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara corridor, Zambia, Tanzania, Kenya, *Power Interconnection,* barabara za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia manufaa ya utaratibu wa *APRM* nchi 23 ikiwemo Tanzania zimeishajiunga. Nchi nyingine Algeria, Burkina-Faso, Cameroon, Jamhuri ya Kongo, Ethiopia, Msumbiji, Ghana, Kenya, Rwanda, Senegal, Uganda, Gabon, Mauritius, Mali, Afrika ya Kusini, Nigeria, Egypt, Benin, Malawi, Lesotho,

Angola na Sierra-Leone. Zambia inatazamiwa kujiunga hivi karibuni. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka saini hati ya kujiunga na *APRM* tarehe 25 Juni, 2004 na Tanzania ikajiunga rasmi tarehe 8 Julai, 2004 wakati wa Mkutano wa Wakuu wa nchi na Serikali ya Jumuiya Afrika Addis Ababa Ethiopia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utaratibu *APRM* unalenga kuboresha utekelezaji wa Mpango wa *NEPAD,* kujenga mfumo wa kuendeleza na kupanua utawala bora na hali ya amani Barani Afrika na kuboresha maendeleo ya watu wa Bara la Afrika kwa ujumla. Naomba sasa niwasilishe Azimio la Kuridhia Mkataba wa Tanzania kujiunga na utaratibu wa *APRM.*

KWA KUWA Tanzania ni nchi moja ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika;

NA KWA KUWA kikao cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika kilichofanyika mwezi Julai, 2002 Durban, Afrika ya Kusini, kilitoa Azimio kuhusu masuala ya demokrasia, siasa na usimamizi bora wa uchumi kwa lengo la kutekeleza kikamilifu mpango wa *NEPAD;*

NA KWA KUWA kupitishwa kwa Azimio hili ni mojawapo ya mikakati ya kutekeleza utaratibu wa *APRM* kwa lengo la kujenga mazingira ya kuwezesha kila nchi shiriki ya *NEPAD* kutekeleza na kuzingatia kwa ukamilifu sera, vigezo na taratibu zinazosaidia kufikia malengo ya *NEPAD;*

NA KWA KUWA Tanzania imesaini makubaliano ya kujiunga na APRM lakini bado haijaridhia;

NA KWA KUWA faida za kuridhiwa mkataba huu ni nyingi ambazo ni pamoja na kuzisukuma au kuzihamasisha nchi za Afrika, kujenga mifumo mizuri ya utawala na siasa yenye uwezo wa kuzuia machafuko na migogoro, kutekeleza sera nzuri ambazo hutoa fursa kwa sekta binafsi, kujenga uwezo wa kupenyeza bidhaa zaidi katika soko la ndani na la Kimataifa kwa ushindani, pamoja na kuiwezesha Afrika kutathmini na kupima utekelezaji wa mambo yake yenyewe pasipo kusubiri Taasisi za nje;

NA KWA KUWA utaratibu wa *APRM* unalenga kuboresha utekelezaji wa Mpango wa *NEPAD;*

NA KWA KUWA ni muhimu kwa Tanzania kuridhia Mkataba huu kwa kuridhiwa na Bunge;

KWA HIYO BASI kwa kutambua umuhimu wa kuridhia Mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge hili katika Mkutano wake wa kumi na nane sasa linaazimia Tanzania kuridhia Mkataba wa kujiunga na utaratibu wa *"African Peer Review Mechanism"* chini ya Mpango wa Ushirikiano Mpya ili kuleta Maendeleo Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA- MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kwa niaba ya wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi na wananchi wa Jimbo langu la Lupa kutoa salaam za rambi rambi kwa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Frank Mussati kilichotokea tarehe 15 Novemba, 2004 kwa ajali ya gari Mkoani Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la mwaka 2004, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha ya Uchumi kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa Tanzania kujiunga na utaratibu wa *African Peer Review Mechanism* Chini ya Mpango wa Ushirikiano Mpya ili kuleta maendeleo Barani Afrika *New Partnership for Africa's Development (NEPAD).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha Azimio la kuridhia Mpango wa *APRM* tulimtaka Waziri aandaa semina kuhusu Mpango mzima wa *NEPAD* kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi. Semina hiyo ilifanyika tarehe 26 Januari, 2005 Jijini Dar es Salaam. Semina iliwezesha wajumbe kuelewa mfumo, muundo na malengo ya *NEPAD* na mantiki ya kuanzishwa kwa *APRM.* Tarehe 1 Februari, 2005 Waziri aliwasilisha Azimio lenyewe mbele ya Kamati na Kamati ilipata muda wa kulijadili na kutoa ushauri waliouona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa wa *APRM* Kamati inaamini kumetokana na uzoefu wa utekelezaji dhaifu wa mipango mbalimbali iliyoanzishwa chini ya *OAU* kwa madhumuni ya kuendeleza Bara la Afrika na watu wake siku za nyuma. Mipango mingi iliyoanzishwa ukianzia na *Legos Plan* haikutekelezwa na hatimaye ilitelekezwa. Hofu ya mipango mizuri kutotekelezwa na nchi za Kiafrika na hatimaye kufa ilifanya viongozi wa sasa tunaamini kujiwekea utaratibu wa kujipima, kujitathimini na kujisimamia wao wenyewe. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha mpango wa *NEPAD* na malengo yake vinatekelezwa na kila nchi mwanachama wa Muungano wa Afrika yaani *AU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hilo *AU* imefanya kujiunga na *APRM* kuwa hiari ingawa utekelezaji wa *NEPAD* ni wajibu wa kila nchi ya Kiafrika iliyotia saini makubaliano hayo. Kamati iliambiwa na Waziri kuwa hadi sasa ni nchi 23 tu zimeridhia au kujiunga na *APRM.* Hatua hii kwa wajumbe ilileta mashaka kwa utayari wa nchi za Kiafrika kutekeleza *NEPAD. NEPAD* imejijengea mfumo wa kujisimamia kupitia *APRM* na nchi inayosita kujiunga na *APRM* inaonyesha haiko tayari kwa dhati kutekeleza malengo na madhumuni ya *NEPAD.* Kamati inaitaka Serikali ya Tanzania au inaishauri Serikali ya Tanzania kupitia makubaliano ya mikutano ya kilele ya Wakuu wa

nchi iendelee kuzichagiza au kuzishinikiza nchi nyingine kujiunga na kutekeleza malengo ya *NEPAD,* kwani Kamati inaamini malengo haya ni mazuri na yana manufaa kwa maendeleo ya nchi zetu za Kiafrika na watu wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya *NEPAD* ya kujenga demokrasia na utawala bora, kukuza na kuimarisha uchumi, kufanya marekebisho ya kuendeleza ushindani wa uchumi katika Afrika, kuondoa umaskini na kuleta maendeleo yakitekelezwa ni ukombozi kwa watu wa Bara la Afrika. Kwa mfumo wa sasa wa dunia utekelezaji wa mambo hayo haukwepeki iwapo Bara la Afrika linataka kuendelea na lisiachwe nyuma katika maendeleo ya kisiasa na kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huo inashangaza kuona kuwa nchi nyingi za Kiafrika ambazo bado zinasita kujiunga na *APRM.* Mabadiliko ya kiuchumi yanafanyika duniani kote hivi sasa. Nchi za Ulaya pamoja na kwamba zimeendelea zinafanya marekebisho katika uchumi wa nchi zao na wanawekeana malengo ya kutimiza. Kwa mfano, katika nchi za Ulaya hata bajeti wanawekeana siri na kwamba deficit isizidi kiwango fulani wanapeana wao wenyewe katika Jumuiya yao na wanalazimika kuzifuata taratibu hizo na nchi ambayo haitekelezi wenzake wanaiuliza kwa nini hufikii hapo.

Kwa hiyo, mimi nafikiri hata sisi katika Afrika wakati umefika kwa kupitia mpango kama huu tuwekeana malengo, tuwekeana utaratibu na tuambizane kwamba wewe kwa nini hutekelezi yanayotakiwa kutekelezwa. Nchi za Kiafrika zisifikiri zinaweza kukwepa malengo ya *NEPAD* na zikaendelea kwa mafanikio makubwa katika ulimwengu wa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa malengo mengi ya *NEPAD* yanaweza pia kutekelezwa Kitaifa. Hili tumeliweka hivyo kwa sababu tumegundua kwamba hata katika Jumuiya ya Ulaya *EU* malengo mengi ambayo ni ya pamoja wanayatafsiri kuyaweka kuwa ni malengo ya Kitaifa, na kwa hiyo wanapotekeleza malengo ya Kitaifa yanaunganishwa na malengo ya *EU.* Kwa hiyo wanapotekeleza malengo yao ya Kitaifa ni moja kwa moja wanatekeleza malengo pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna haja ya kusubiri yatekelezwe kama programu maalum. Njia nzuri ya kutekeleza malengo ya *NEPAD* ni kuyatafsiri kwenye mipango ya Kitaifa yale yote yanayoweza kuingia kwenye ngazi hiyo. Ni malengo yale tu ambayo yanahitaji ushirikiano wa pamoja na nchi nyingine za Kiafrika ndiyo yanaweza kusubiri mpango wa *NEPAD* kama programu. Kamati ilimweleza Waziri kuridhika kwake na Serikali ya Tanzania kwa kuwa na malengo ya *NEPAD* mengi tayari yanatekelezwa hapa Tanzania. Tunashauri Tanzania iendelee na utekelezaji wa programu hizo kwa nguvu zaidi na umakini zaidi. Kukuza uchumi na kujenga demokrasia na kuleta utawala bora si masuala ya kusubiriana, Tanzania iongoze njia na iache wengine wafuate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujenga demokrasia si suala tu la kuwa na vyama vingi na kupanga uchaguzi, suala la demokrasia linahitaji kuwa na uchaguzi huru na wa haki na tuepukane na mizengwe. Nchi nyingi za kiafrika baada ya kupatana

wenyewe kwa wenyewe na baada ya kukumbana na Mataifa mengine tumefungulia milango ya demokrasia, lakini tunakuwa na mizengwe mingi katika uchaguzi kiasi kwamba wananchi wanashindwa kuchagua viongozi wao wanaowataka kutokana na mizengwe inayoanzishwa. Kama tumekubali mfumo wa demokrasia, basi tuendelee na utaratibu kama unavyotaka.

Mpango mzima wa *NEPAD* unahitaji fedha nyingi karibu dola za Kimarekani milioni sitini na nne. Kiasi hiki siyo rahisi kukipata hata wafadhili wenyewe wamekwisha utaja mpango wa *NEPAD* kama ni *ambitious*. Aidha, wafadhili wengi wamesema hawawezi kuchangia *NEPAD* mpaka nchi za kiafrika zifanye marekebisho ya kiuchumi, utawala bora, kuleta sera zinazoambatana na uchumi wa soko na kuondoa rushwa. Haya si mambo yanayoweza kufanyika haraka katika nchi nyingi za Kiafrika, kwa hiyo *NEPAD* haitazamiwi kuanza kikamilifu hivi karibuni.

Kamati inaishauri Serikali iendelee kupanga na kutekeleza *program* zake kama sehemu ya mkakati wake wa kubadili uchumi wa Tanzania, kuleta utawala bora na kuondoa umaskini ndani ya Tanzania. Kuna hatari ya miradi kupelekwa *NEPAD* na kusahaulika huko. Kamati inashauri kwamba, tuendelee kuitekeleza miradi yetu sisi wenyewe na itakapoonekana kwamba sasa mambo ni tayari ndipo tuweze kusema tunaipeleka *NEPAD*. *(Makofi)*

Hata hivyo, Kamati inazipongeza nchi za Kiafrika kuja na kuandaa na kuja na mpango wa *NEPAD* ambao tunadhani utaimarisha udhibiti wa masuala yanayotuhusu Afrika na Waafrika wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inamshukuru Waziri kwa kufanya Semina, kupokea ushauri wake na kuufanyia kazi. Ninampongeza yeye, Katibu Mkuu Dr. Enos Bukuku na wataalam wao kwa ushirikiano waliyoipa Kamati wakati wa kujadili Azimio. Aidha, nawapongeza Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Azimio na kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe ili kuruhusu utekelezaji wake. Naunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou.

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kifungu cha 43 kifungu kidogo cha 5(b) na 81 (1) toleo la 2004 kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Tanzania Kujiunga na Utaratibu wa *African Peer Review Mechanism* chini ya mpango wa *NEPAD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kusema lolote, kwa niaba ya Wapigakura wangu wa Kigoma Mjini, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa wananchi na familia ya Marehemu Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki. Mungu aiweke pema roho yake Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kuwa Bara la Afrika watu wake wanakabiliwa na njaa, umaskini, elimu duni, ujinga, maradhi na kwa sasa hasa gonjwa hili hatari la Ukimwi. Aidha, Bara la Afrika linakabiliwa pia na rushwa, vita, madeni makubwa na uongozi wa kibabe. Serikali nyingi za Afrika zilichukua hatua kadhaa za kujiletea matumaini katika siku zilizopita kama vile ubinafsishaji na marekebisho ya sera mbalimbali, lakini bado hali haijaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya nchi moja moja kushindwa mipango yao, Viongozi wetu wa Kiafrika walichukua jitihada za kuanzisha mpango maalum wa ushirikiano ili kuleta maendeleo Barani Afrika na mpango huo kama tulivyosikia ndiyo huo unaoitwa *NEPAD*, ambao kwa kweli lengo lake kuu ni kuondoa umaskini kwa kupitia nyanja tofauti. Kwa mfano, kuzuia migogoro na mapigano Afrika; kuimarisha sera zetu za kiuchumi na kujamii; kuwapa uwezo wanawake katika masuala ya huduma, uchumi, elimu na vile vile kuboresha miundo mbinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza malengo yake hayo ya *NEPAD,* Serikali zetu za kiafrika zimekubaliana kuweka utaratibu wa kuhakikiana, yaani *African Peer Review Mechanism.* Utaratibu huu ni wa hiari kwa kila nchi inayokubaliana nao, lakini Kambi ya Upinzani ingependekeza kwamba utaratibu huu usiwe wa hiari, uwe ni utaratibu ambao unaziwajibisha nchi zetu katika kuwatetea au kutetea maslahi ya Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikiwa kwa malengo ya *NEPAD*, Afrika kwa sasa inatilia mkazo uwekaji wa mazingira bora ya kuleta maendeleo endelevu, yaani *sustainable development*. Nchi zote shiriki za *NEPAD* zitawajibika kutekeleza na kutoa taarifa ya utekelezaji katika vigezo vyote kama ilivyoainishwa katika malengo ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inashukuru na kuliomba Bunge kuridhia Mkataba huu kwani nchi yetu imeshatekeleza mambo mengi ambayo ni malengo ya uanzishwaji wa *NEPAD* na tumeyasikia. Hata hivyo, tunadhani kwamba katika suala la siasa bado Tanzania tuna tatizo na suala zima la Mfumo wa Vyama Vingi, kwani pamoja na kukubali Mfumo wa Vyama Vingi bado taratibu za utekelezaji wake zinasuasua. Mfano hai ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo kwa kweli mpaka sasa siyo huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu ya kutokuwa na Tume Huru ya Uchaguzi inayoshughulikia chaguzi katika ngazi zote tangu Taifa hadi Mtaa yanapelekea utaratibu wa uchaguzi ambao kidogo kidogo tunaona unatupeleka kwenye vurugu na mauaji kama yalivyojitokeza Dar es Salaam na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mdharau mwiba mguu huota tende. Tunadhani kupuuza muundo wa Tume ya Uchaguzi kunaweza kusababisha mafanikio makubwa ambayo tumeyaona kimiundo mbinu, MEM, MMES na mengine yote kama Tume ya Haki za Binadamu yaliyofanywa na Serikali yakisambaratika kirahisi kutokana na vurugu zinazoweza kujitokeza. Vile vile, tunaona pungufu lingine katika suala zima la uwiano

katika mfumo huu wa Vyama Vingi kwani pamoja na kwamba tuko kwenye Mfumo wa Vyama Vingi lakini kikatiba mfumo huu bado haujatambuliwa vilivyo. Tunaona kwa mfano Ofisi ya Waziri Mkuu na viongozi wengine ikiwa imetajwa moja kwa moja katika katiba yetu, lakini Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani ambaye kwa vyovyote atakuwepo muda wote, haitajwi popote kisheria wala kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kukagua na kupima utekelezaji wa malengo ya *NEPAD* katika nchi mwanachama uitwao *African Peer Review Mechanism* ulioanzishwa na nchi husika, unatakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji katika nyanja mbalimbali. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa ni vigumu kwa *APRM* kutimiza majukumu yake kulingana na mazingira yanayotawala kwenye Serikali nyingi za nchi zetu za kiafrika. Utaratibu wa kuhakikiana wenyewe kwa wenyewe ili kuona kama malengo ya uanzishaji wa *NEPAD* katika nchi husika yanafuatwa unaweza kuwa ni mgumu sana kwani misingi ya hayo yote ni jinsi gani viongozi wetu wameingia madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kiongozi ameingia madarakani kwa njia ya rushwa, ni wazi kabisa kuwa hawezi kupambana na rushwa. Vile vile, ikiwa ameingia madarakani akitokea msituni, basi hatudhani kwamba kiongozi huyu anaweza kutetea demokrasia. Kwa mfano, kuhusu suala la rushwa katika nchi yetu hakuna hata kiongozi mmoja hapa Bungeni na kwingineko anayekataa kukithiri kwa suala hili nchini kwetu. Lakini bado hata katika Bunge letu tunaweza tukaambiwa kabisa kwamba Mikataba kati ya Serikali na Mashirika ya nje ni siri na sisi tunakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Bunge hili liridhie Mkataba huu ili na sisi tuweze kukaguliwa na kushauriwa tufanye nini katika kuokoa Taifa letu toka kwa watu wenye uchu wa kujitajirisha haraka haraka. Utaratibu huu wa kuhakikiana kwa viongozi wetu wa kiafrika, *Africa Peer Review Mechanism* unalenga kuziwajibisha dola zote za kiafrika kujihusisha kuelewa kile kinachoendelea katika nchi nyingine za kiafrika na pale ambapo hapana budi nchi hizi kuwajibika kwa pamoja kutafuta ufumbuzi wa matatizo yao kwa pamoja, kuziondoa kasoro zile na hata kuongezea uwezo pale penye mapungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu na malengo ni mazuri na tunawapongeza waasisi wa mawazo hayo. Lakini kama Kambi ya Upinzani, tunaamini kuwa chombo au mamlaka yenye uwezo wa kuiwajibisha dola yoyote inayoenda tofauti na malengo ya *NEPAD* ni wananchi wa nchi husika waliouweka madarakani Uongozi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa utaratibu wa *APRM* uwahusishe vile vile tena moja kwa moja wananchi wa nchi husika katika tathmini zake ili kwa kweli kama tunavyofanya sasa Tanzania wadau wote wawe wanajua kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache, napenda kusema moja kwa moja kama nilivyokwishadokeza huko nyumba kwamba Kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio hili na tunapenda litekelezwe haraka iwezekanavyo. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge Wasemaji Wakuu wamemaliza kuwasilisha. Kabla sijawataja wale waliomba ningependa ku-*share* ki-*note* nilicholetewa hapa wakati hawa Wasemaji Wakuu watatu wanazungumza, mmoja wetu akaandika, "Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tumekubali haya yote ya *NEPAD.* Haya maneno mengi ya nini? Si utuhoji tu tuondoke. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini sasa ningependa kumjulisha yeye na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tunao Wasemaji wanne ambao watachangia halafu Mheshimiwa Waziri tutamruhusu aweze kumalizia. Msemaji wa kwanza ni Mheshimiwa Dr. Milton M. Mahanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Anne S. Makinda, atafuata Mheshimiwa Remidius Kissassi na mwisho Mheshimiwa Dr. Abdullatif Hussein Esmail. Sasa namwita Dr. Mahanga.

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kunitetea ki-*note* hicho kingeweza kuniondoa. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kwanza ya kuchangia mjadala wa jumla kwenye hoja hii iliyopo mbele yetu. Lakini kabla ya hapo na mimi niungane na wenzangu kutoa rambirambi zangu nyingi sana kwa Wapigakura na familia ya Marehemu Frank Michael Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki ambaye kwa kweli kwa wengine sisi tulikuwa naye jirani hapa na kwa kweli imetugusa sana na tunamwomba Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niende sasa moja kwa moja kwenye hoja hii na nitangulize pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kuweza kuleta hoja hii Bungeni ili tuweze kuridhia Tanzania kuingia katika mpango huu wa *APRM* chini ya mpango mkubwa wa *NEPAD*. Niseme toka mwanzo kabisa kwamba kwa wengine wetu tunaona kwamba tumechelewa. Kwa kweli kwa nchi kama Tanzania kuwa ya 20 au ya 22 kujiunga na mpango muhimu kama huu, tunaona kwamba tumechelea, lakini mradi Serikali sasa imeleta hoja hii, basi tuipongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme wazi kabisa kwamba kwa sisi wengine ambao tumekuwa na nafasi ya kutembea nchi zingine za kiafrika, kabla ya Juni mwaka jana, 2004 tulikuwa wakati mwingine tunashindwa namna ya kujieleza tukiambiwa kwamba kwa nchi kama Tanzania ambayo wenzetu wengine wa Afrika wanaamini na nadhani wanaamini kisahihi kwamba tuko mbele sana kwa masuala ya utawala bora ya kusimamia uchumi wetu na kuendeleza utawala wa kisheria, kwa nini tunasita kwa muda mrefu mpaka karibu nchi ishirini zingine ambazo zilikuwa hazitegemewi kwamba zina utawala bora kama sisi au zinasimamia uchumi zikawa zimesharidhia? Wengine tulikuwa tunashindwa kujibu kwa sababu hatukuwa na hiyo *mandate* ya kujibu, lakini na sisi ilikuwa inatusikitisha.

Kwa hiyo niseme kwamba kwa kweli tumefurahi kwamba sasa angalau tumeleta na nasema hivyo kwa sababu Tanzania ni nchi mojawapo ambayo toka mwaka 2001 tumeridhia suala hili la *NEPAD* kama mpango ambao unatuwezesha kama Waafrika kuinua uchumi wetu kuendeleza utawala bora na kupunguza au kuondoa kabisa umaskini. Sasa mpango huu wa kupimana ulipozinduliwa tukawa tunaona kwamba Tanzania inasita

ikawa kidogo inatuchanganya. Ninasema hivyo kwa sababu kama nilivyosema, nchi yetu tumepiga hatua pamoja na dosari ndogo ndogo ambazo zipo ambazo zinazungumzwa lakini siyo nchi ambayo unaweza ukasema ni ya 20 kwa utawala bora Afrika, hata kidogo! Labda itakuwa katika nchi tano bora na tungetegemea tungekuwa kati ya watano wa kwanza wa kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme kwamba kabla ya kulizungumza suala zima la mpango huu wa kujihakiki wenyewe kwa wenyewe wa Afrika katika mpango wa *NEPAD* ni vyema tukaelewa mpango mzima huu wa *NEPAD* na faida zake na tujiulize kwamba; je, wananchi wanaelewa kwamba hawa Wabunge wanaporidhia hiyo Mikataba, huhakiki chini ya mpango unaoitwa *NEPAD*? *NEPAD* yenyewe hiyo kwanza ni nini?

Nasema hivyo kwa sababu, ukiangalia na ukitembea kwenye Majimbo na mimi hata kwenye Jimbo langu ambalo wajuaji wa Jijini Dar es Salaam ni wengi sana, Wapigakura hawaelewi hii *NEPAD* ni nini na wameweza kuisikia tu ni mnyama gani. Lakini kubwa zaidi hata kwa wale wanaoijua faida yake ni nini na inatutaka tufanye nini kama sisi wananchi; Je, ni kwa ajili ya nyie viongozi, Wabunge, Mawaziri na Marais au na sisi wananchi tunahusika kwa namna moja au nyingine? Wanauliza maswali hayo.

Kwa hiyo ni vyema basi, pamoja na kuridhia mpango huu wa *APRM,* mpango mzima wa *NEPAD* ukaendelea kuelimishwa kwa Wapigakura, wananchi, wadau mbalimbali ili kila mmoja ajue vizuri hii *NEPAD* itasaidiaje Tanzania na Afrika na kubwa zaidi mimi kama mwananchi jukumu langu ni nini katika kuendeleza mpango mzima wa *NEPAD*. Kwa kweli wananchi hawaelewi kwamba haya ambayo tunayafanya katika mpango wa kuondoa umaskini Tanzania, mpango wa kufikia malengo yetu ya maendeleo yote hayo yanatekeleza mpango wa *NEPAD*.

Hawaelewi kwamba mpango wa *NEPAD actually* unaanzia kutoka Kijijini, kwa hiyo unapokuza kilimo chako Kijijini, kukiwa na huduma za jamii, masuala ya miundo mbinu, biashara, viwanda na kadhalika katika ngazi ya Kijiji, ukaunganisha mipango hiyo na mipango ya Wilaya kwa mfano na ya Wilaya ikaunganishwa na ya Taifa, ndipo unapoweza kuunganisha hiyo ya Taifa na Mataifa ya kiafrika na ukapata sasa mlolongo wa kutekeleza mpango wa *NEPAD* kwa nchi za Afrika. Kwa hiyo mipango hii yote ya *NEPAD* haiwezi kutekelezwa kule juu kwa ngazi za Taifa kama haijaanza kwenye ngazi ya chini. Sasa wananchi walielewe hilo kwamba unaunganisha mipango hiyo kutoka chini hadi juu Taifa na Taifa tunaunganisha kwenye mahusiano na nchi nyingine, basi tunaweza kufanikiwa.

Lakini hata kwenye utawala bora, unapozungumzia kupiga vita rushwa kwenye ngazi ya Kijiji au kuwa na haki za raia kwenye ngazi hiyo, unapozungumzia masuala ya demokrasia, uchaguzi wa Serikali za Mitaa kama umefanywa kidemokrasia, kama kuna amani na utulivu, hivyo hivyo ikipanda ikafika ngazi ya Jimbo ikaendelea ngazi ya Taifa, ikaunganishwa na Waafrika wakafanya, basi unapata utawala bora unaozungumzwa. Sasa inatakiwa kwa kweli wananchi walielewe hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema kwamba *NEPAD* ni mpango mzuri na mimi sitaki kuzungumzia matatizo yaliyokuwepo na ubishi ambao umekuwepo kwa

muda mrefu na bado upo kwamba *NEPAD* siyo mpango uliyobuniwa na viongozi wetu wa kiafrika. Mimi nina mawazo tofauti, lakini hata hao ambao walikuwa na mawazo kwamba huu mpango kwa namna moja umeshinikizwa na Mataifa makubwa ni lazima sasa wakubali kwamba sisi kama Waafrika hata kama ulileletwa, basi tumeshauchukua, tumeuboresha na tunataka kuutekeleza kwa mikakati ambayo tumejiwekea, basi wakubali na twende mbele badala ya kubishana kwamba umeshinikizwa. Sasa kushinikizwa haitatufikisha mbali, tumeshaelezwa jinsi *NEPAD* ilivyoanza.

Lakini kitu nilitaka nikieleze ambacho nitakiunganisha na mpango wa APRM ni kuelewa *NEPAD* na hizi nchi tajiri uhusiano wake uko wapi. Uhusiano mkubwa ambao upo na ndiyo maana tumeelezwa kwamba wale viongozi wetu wakubwa ambao kwa kweli tuliwapa *mandate* hiyo, wakina Obasanjo na wenzake na Mbeki kwamba waende kwa nchi hizi tajiri na wajaribu kuzungumza nao kuhusu hali ya Afrika hasa kuhusu kupunguziwa madeni na namna gani wanaweza kuingiza mitaji katika nchi za kiafrika, hizi nchi tajiri zitatusaidiaje katika kutekeleza mipango yetu ya kuondoa umaskini?

Kwa hiyo katika majadiliano na nchi zile tajiri ndiyo tutaanzisha mpango wetu na tunataka nyie mtusaidie kuutekeleza. Kwa hiyo ni mpango ambao unatekelezwa kwa ubia kati ya Waafrika kutumia rasilimali zao na wale nchi za nje. Hapo ndipo wakasema, ili tuweze kutekeleza pamoja na rasilimali zetu, nchi tajiri lazima ziingize Afrika kiasi kinachofikia dola bilioni 64 za Kimarekani. Kwa hiyo hapo sasa ndiyo unaona uhusiano unakuja kwamba kama hayo ndiyo makubaliano, hao wakubwa wanasemaje, kwamba sawa sisi tuko tayari kusaidiana na nyie katika mpango wenu mkubwa huo mliobuni na ambao tumeuboresha kwa sababu katika kuuboresha kwa kweli nchi tajiri na Mashirika mengi ya ulimwengu yalisaidiana na Waafrika kuutengeneza.

Sisi tunachotaka ni kwamba na nyinyi kama Waafrika na Serikali zenu, basi muweke utawala bora msimamie uchumi wenu vizuri nasi tutaleta hiyo mitaji ambayo inahijika kujenga uchumi wenu. Ndiyo makubaliano yaliyopo na ndiyo uhusiano uliyopo kwamba sisi tusimamie uchumi vizuri, na hii wanasema wameliweka kwa faida yao kwa sababu wakiwekeza Afrika watataka wawe na hakika ya huo mtaji wao. Kwa hiyo wakiweza sehemu ambapo utawala bora haupo au uchumi hausimamiwi, kuna hatari mitaji yao ikapotea. Kwa hiyo ndio maana na wenyewe wanasema nikutusaidia na wenyewe kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mpango wa *APRM* ingawaje sio *condition* ya kutusaidia ya kuleta hizo bilioni 64 ndiyo maana inashangaza kwamba wengine kwa kweli wanaonekana hawataki kuingia, lakini kwa kweli wanaogopa kutokana na utawala bora ambao haupo labda kwenye nchi zao au kuwa na wasiwasi namna wanavyosimamia uchumi wao. Kwa taarifa zilizopo ni kwamba, nchi ambazo zitakuwa zimeshapimwa kwa sasa hivi fedha zipo nyingi ambazo zinataka kuingizwa na wawekezaji kupitia mpango huu wa *NEPAD*. Lakini wanangojea matokeo ya sisi kupima na kwa hiyo nina hakika kwamba baada ya sisi kukubali hili na tukapimwa, nadhani baada ya hapo muda mfupi watakuja kupima Tanzania. Hapo tutakuwa na nafasi nzuri sasa ya kuingiza hiyo mitaji kutoka nje kwa maana ya uwekezaji lakini kwa mpango huu mahsusi tutapata mitaji mikubwa zaidi kulinga na utaratibu uliopo.

Kwa hiyo, kwa upande mwingine ni shinikizo lakini upande mwingine unatusaidia na mimi ndio maana nasema nakubaliana na wenzangu kwamba ni vyema nchi za kiafrika kama zinataka zifaidike kwa ujumla katika mpango ule wa *NEPAD* na nina hakika misaada hiyo itaanza kwa wale walioanza kujipima kwanza ndio utaratibu uliopo ingawaje hauko wazi. Lakini wamejiandaa kuleta kwanza kwa wale waliojipima na ni vyema wote tukakubali nchi za kiafrika na kwa hiyo tuwaambie viongozi na hasa hawa wa nchi 23 ambao wameshaingia wawashinikize na wenzao ili Afrika kwa ujumla tuweze kuwa katika mkakati mmoja wa kuweza kutekeleza *NEPAD* kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kuzungumza ni nafasi gani Wabunge sasa kama wadau tunayo? Siyo kupitisha tu, lakini namna gani tunaanza na tunaendelea kushawishi wananchi waelewe vizuri *NEPAD* na hiyo *APRM* na namna gani tunaisimamia Serikali yetu iweze kutekeleza hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimependekeza kwamba, lazima tuwe na Kamati maalum ya *NEPAD* Bungeni ambayo ni tofauti na hizi Kamati nyingine ambazo ni *pressure cooked,* Kamati ambayo itakuwa inatoa taarifa zake Bungeni na inajadiliwa ndani ya Bunge bila kupitia Kamati yoyote ya *Standing Committee.* Kamati zote zitoe watu kadhaa ili Kamati hiyo maalum ya *NEPAD* ianze ambayo itasaidia. Nchi nyingine za kiafrika zimefanya hivyo ambao wameshakuwa mbele katika utekelezaji wa *NEPAD* wanazo hizo *NEPAD, Working, Parliamentary Groups* na sisi lazima tufuate mpango huu. Kwa sababu hii, sasa ndio itakuwa *watchdog* ya kuishinikiza Serikali., Serikali inapotoa, tunaleta Bungeni tunaihoji Serikali na tunatoa mapendekezo yetu ili Serikali iweze kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii na naomba kwa kweli wenzangu wote tuunge mkono ili tupitishe kwa sababu ni mpango ambao utasaidia uchumi wetu. Naomba kuunga mkono. (*Makofi*)

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naomba niwatakie wenzangu heri ya mwaka mpya na pia naomba nitumie nafasi hii kutoa salamu zangu za rambi rambi kwa Mheshimiwa Mbunge, Frank Michael Mussati ambaye alikuwa rafiki wa kila Mbunge aliyopo hapa. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema aliyekuandikia ki-*note,* ni kweli ingependeza sana ukapitisha bila mjadala. Lakini nadhani katika Bunge tunavyoongea ni sehemu pia ya kujifunza kutokana na sisi kwa sisi. Naomba nimshukuru Waziri kwa kuleta Azimio hili mimi binafsi kama alivyosema ndugu yangu Dr. Mahanga hapa. Kweli tulikuwa tunashangaa kwa nini sisi Tanzania hatuingii katika mkakati wa *APRM*. Tulikuwa tunashangaa kwa sababu hata wenyewe walikuwa wanatuuliza kwamba hivi Tanzania kwa nini? Mfano ni hotuba aliyotoa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juzi wakati wa Mkutano wa Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano wa Maziwa Makuu, Mheshimiwa Rais alipotoa hotuba yake, viongozi wengi wa Maziwa Makuu walikuwepo hapo, Rais alitoa hotuba kali sana ambayo ilikuwa ni ya kujikosoa sisi wenyewe viongozi wa Afrika kuhusu vitendo vyetu kwa kuviendeleza vita, kuendeleza vitendo vya rushwa na vitu kama hivi. Sasa sisi tukawa sio *members* wa hii kitu na kiasi fulani ilionekana kuna kitu ambacho sio cha kawaida na sisi wengine kweli tukawa tunashangaa kwa nini Serikali inatia wasiwasi kuhusu suala hili. Tukawa tunashangaa labda Rais anangoja aondoke yeye halafu atakayekuja ndio aingie huku. Kwa sababu ni kweli katika *APRM* ipo hii Kamati aliyotaja Waziri, inakuja kuzamia katika nchi hii na kufuatilia vitu vichache vichache pamoja na mambo ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanakuja kuchunguza jinsi mnavyotekeleza mambo ya kupambana na rushwa, jinsi mnavyotekeleza mambo ya jinsia, ndiyo maana mnakuta ile Kamati wako watu watano. Nafikiri watatu ni akinamama pale. Ni mambo ambayo yanakuja kuzamia nchini hapa. Hata kama Mheshimiwa Dr. Kigoda amesema kuna nchi zaidi ya 20 na kitu zimeridhia, lakini ambazo hii Kamati imekwenda ni Ghana, Rwanda pia watakwenda, Kenya wameomba ndio wameanza na Uganda. Kwa hiyo tunashukuru sana kwamba suala hili na sisi angalau tuna mahali pa kusemea.

Kwa hiyo suala la ARPM hili ni namna ya nchi yenyewe inavyojidhibiti yenyewe lakini na wengine wanaidhibiti pia. Kwa hiyo mimi naamini ni njia iliyo hakika ya kwamba wananchi wanaweza kuridhika kwamba nchi yenu inakwenda kufuatana na viwango ambavyo nchi za Kiafrika zimekubaliana na zimejiwekea zenyewe utaratibu hu. Kwa sababu wakati mwingine tunapodhibiti sisi wenyewe hatuaminiani kwa sababu hujui ni kwa kiwango gani. Ndiyo maana unakuta mara Serikali ikisema, tunasema aah, si kweli haya mliyosema. Lakini kama mtu wa nje atakuja kuangalia na kusema kwamba kweli Tanzania wanafanya moja, mbili, tatu, nne, inaleta imani hata kwa wananchi wengi kwamba kumbe Serikali yetu ipo katika mstari ulio sahihi na nchi nyingine. Kwa hiyo mimi nasema hili jambo ni zuri, tena zuri sana na tunashukuru hii imefanywa kwa wakati huu. Sasa kabla hujataka watu wa kuangalia, unatakiwa ufagie nyumba yako. Kuna sababu gani ya kuwaalika watu waje kuangalia wakati wewe mwenyewe hujaanza kufagia? Uanze kufyagia humu humu kwanza! Sasa mambo ambayo yanatakiwa kufagiliwa humu ndani yapo.

Kwa mfano sasa hivi Tanzania kama hatuangalii tunaanza kuingia kwenye siasa isiyokuwa ya uvumilivu wala kuvumiliana. Sisi wote ni Watanzania tumezaliwa ndani ya nchi hii na tuna haki zote za kuweza kufuata utawala na kuingia katika uongozi. Kwa nini inakuwa viongozi wengine hawapendi kuwa wavumilivu na kulinda amani? Kwa nini? Ukiwauliza sababu zake hata ukiwasikiliza, kiongozi mkubwa mwenye madaraka anadhubutu kukaa mbele ya hadhara na kusema uongo kabisa na yeye mwenyewe anaamini anasema uongo. Inashangaza kweli kiongozi mkubwa wa Chama anasimama kwenye majukwaa kusema uongo na kuwachanganya Watanzania kwa sababu zake mwenyewe. Hii inatoka wapi? (*Makofi*)

Mimi nasema huu nao ni udhaifu. Kama unataka uongozi, sema ukweli watu wakuamini na wakushiriki, lakini kusema uongo unawachanganya watu. Kwa hiyo mara

nyingi unakuta viongozi kweli kabisa kwa maslahi ya kisiasa kwao wenyewe wanasema uongo mbele ya hadhara. Sasa vitu vya namna hii ni maeneo ya kujidhibiti wenyewe.

**MBUNGE FULANI:** Udumu Mwenyekiti!!!!!

**MHE. ANNE S. MAKINDA:** Kwani mimi ni *APRM*? (*Kicheko*)

Kwa hiyo hiki ndicho tunachokisema, lakini kuna mengine. Maneno kama haya tunayozungumza kila siku, kwa mfano rushwa, hivi unakwenda kuwakaribisha watu huku unafahamu kuna maeneo mengi mazito ambayo hayajakwenda vizuri. Kwa nini ukubali ungoje mpaka waje wao? Kwa nini usijisafishe wewe mwenyewe kabla? (*Makofi*)

Kuna maeneo kwa mfano kwa nchi nyingine sasa kung'ang'ania madaraka. Sasa hivi angalau hilo linaanza kwishakwisha kung'ang'ania madaraka kwa viongozi, kutaka mtu aendelee na aendelee, hilo nalo ni tatizo. Kwa hiyo katika mfumo mzima wa *NEPAD* unaweza kutafsiri *NEPAD* unavyotaka wewe, lakini ukweli mpango wa *NEPAD* ni mpango wa nchi za kiafrika katika kujiletea maendeleo endelevu kwa kushirikiana na kujifunza kwa wale waliofanya vizuri kuliko wengine na kushirikiana kuweza kuyatumia yale mafanikio ya nchi nyingine katika nchi zetu. Ndiyo maana ya *NEPAD* kwa kifupi naweza kusema hivyo. Kwa Tanzania kama tulivyosema, tujifunze kwa mambo mazuri ambayo nchi fulani imefanya ili na nchi nyingine iweze kuiga, ni jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi leo Mheshimiwa Waziri hapa ameanza kuorodhesha kwamba Tanzania tumeshafanya hivi, tumefanya hivi, kwa hiyo naomba hayo mambo mazuri mnayofanya yaendelee kutamkwa. Yapo mengi sana! Tusianze kuamini kuwa watu wanajua, tusifanye hivyo. Serikali izungumze kwa sababu hii *good practice* na watu wengine wajue Tanzania tunafanya nini. Kwa mfano MMEM. MMEM tumefanya makubwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetembea nchi nyingine za kiafrika hakuna cha MMEM wala nini. Ni vizuri tukaendelea kutamka wakati wote na watu wetu waweze kujua na kuridhika. Kwa mfano kwenye Jimbo langu, wananchi wasidhani kama wanavyohangaika kujenga shule labda ni wao peke yao. Mkisema kwamba wengine pia wanajenga, inaonekana kwamba kumbe sisi hatufanyi kitu ambacho sio cha kawaida. Kwa hiyo tutamke mafanikio haya na ni sehemu ya *NEPAD*.

Kama alivyosema Dr. Kigoda, tukianza kutamka *NEPAD* haiwi kama ni suala zito kama wanavyozungumza nchi nyingine ooh, *NEPAD* imetoka Ulaya, imetoka Ulaya; haijatoka Ulaya, ni yetu sisi wenyewe tuyatamke mambo ya *NEPAD*. *NEPAD* kazi yake moja ni kuhakikisha nchi zetu hizi tunapata elimu ambayo inaweza kutupeleka kwenye mambo ya Sayansi na Teknolojia. Mambo ya *NEPAD* ni kuondokana na magonjwa yasiyokuwa na lazima kama *TB*, UKIMWI na magonjwa ambayo tunaweza kuyazuia kama Malaria. Vitu kama hivi tupambane navyo! *NEPAD* ni kupambana na umaskini uliobobea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu Umoja wa Mataifa umetangazwa kwamba ni mwaka wa *Credit* na *Microfinance,* yaani mikopo na Mifuko midogo midogo kwa wananchi wa kawaida. Huu ndiyo mwaka wake. Sasa unaweza ukapita mwaka watu tusijue hata kama ni mwaka wa namna hiyo. Kama tunajua; Je, Tanzania tumejizatiti kiasi gani kwamba na sisi katika mwaka kama huu wa kupambana na umaskini ni mwaka wa *Credit* na *Microfinance* tunaweza kufanyaje? Kama tunafanya tunaweza kuratibu na kuweza kueleza kipindi fulani kwamba tumefanya hivi, tusiache hotuba za kisiasa.

Hapa suala la umaskini ni suala la kweli ambalo wananchi wetu wanalo. Tuache kuzungumza kisiasa, tuseme watu wangapi na tuna mpango gani rasmi wa kutoa mikopo kwa wananchi wadogo wadogo, mikopo kwa wanawake, vijana, walemavu na mikopo kwa watu ambao mazingira yao ni magumu. Huu ni mwaka wa Umoja wa Mataifa, sasa sisi tutaweza kusemaje tutakapomaliza mwaka? Huu ni mwezi Februari, ningependa Serikali ijidhatiti katika maeneo kama hayo. (Makofi)

Tunaishukuru Serikali kwa kutoa ruzuku kwenye pembejeo. Kwa kweli mimi nilikuwa mlalamikaji mmojawapo mkubwa kabisa kwa sababu katika Jimbo langu bila pembejeo hujasema kitu. Kwa hiyo naishukuru Serikali na hususan Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Keenja kwa kuchukua jukumu la kuhakikisha mbolea kule imefika na imegawiwa vizuri kwa mtindo wa ruzuku. Mimi sina malalamiko na naomba sana nishukuru. Kwa hiyo naunganisha na hilo kwamba ni sehemu ya kupambana na umaskini katika masuala ya kutoa mikopo midogo midogo. Ukiweza kumpunguzia mwananchi bei ya mbolea akapata kwa bei ambayo ni nafuu anayoweza kuitumia akalima vizuri, pia itamsaidia kuondokana na umaskini.

Kwa hiyo mimi ninatumia nafasi hii kusema kwamba jamani *APRM* ni jambo zuri la kuweza kusaidiana na nchi nyingine. Nchi nyingine wakuangalie! Mtu akichukua kioo atajiona usoni lakini kisogoni hawezi kujiona. Hii *APRM* ni kama kioo kusema bwana kisogo chako bado hakijakaa vizuri. Kwa hiyo mimi hii naipongeza. Pia, naishukuru pia Serikali kwa kweli kwa mbolea ambayo imefika katika Jimbo langu kwa wingi na wananchi wameitumia na naomba niishukuru Serikali. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipa fursa hii. Lakini vile vile nikutakie wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kheri ya mwaka mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kuungana na wenzangu kutoa mkono wa rambirambi kwa ndugu na jamaa kwamsiba mkubwa walioupata kwa kifo cha ndugu yetu Frank Mussati, ambaye alitutoka mwezi wa Novemba 2004. Mungu amlaze mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa kutuwasilishia hoja hii ambayo kama walivyosema wenzangu, nafikiri imechelewa kidogo lakini heri kuchelewa kuliko

kutokufika kabisa. Kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Waziri na tunaomba sasa hili suala la *NEPAD* na *APRM* alifanyie kazi kwa bidii sana.

Ni kweli kuwa masuala ya *NEPAD* yameasisiwa na viongozi wetu wa Afrika kwa ajili ya Waafrika na tunatakiwa sisi wenyewe tuwe mstari wa mbele kama wadau muhimu kuutekeleza. Kwa hiyo lazima tuchukue jitihada zote kuanza kuelimisha jamii nini hasa mpango huu wa *NEPAD*. Jamii ya makundi mbalimbali, wafanyabiashara, akinamama, vijana, walemavu, Serikali, *NGOs* na kadhalika wote wana nafasi ya kushiriki katika mpango huu wa *NEPAD* ambao malengo yake makubwa ni kuinua uchumi wa Afrika na kubadilisha mwelekeo wa Afrika kutoka umaskini uliokithiri sasa hivi na kuinua hali ya maisha ya wananchi. Waafrika tumechoka kila wakati kuonekana tuko nyuma. Maradhi yote ni Afrika, elimu mbovu ni Afrika, barabara mbovu ziko Afrika, ilimradi Waafrika tuko nyuma. Kwa hiyo ni wakati muafaka sasa hivi kutia gear tuelekee mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala la *NEPAD,* mipango kama tutaifanya vizuri tukairatibu na hili naomba Mheshimiwa Waziri aweke Kitengo cha Kuratibu Masuala ya *NEPAD* katika Wizara yake haraka sana kwa sababu utaratibu unaotakiwa ni kuwa hiki kitengo cha Kuratibu Masuala ya *NEPAD* kishirikishe jamii za aina zote isiwe ni Serikali peke yake. Kwa hiyo wawepo wafanyabiashara, akinamama, viwepo vikundi vingine vyote ambavyo ni wadau na wabia katika masuala ya maendeleo ya nchi yetu. Tusikubali suala hili la *NEPAD* likawa na masuala ya kisiasa ambayo yatatturudisha nyuma. Sisi tuangalie suala hili kama Wazalendo na kama Waafrika ambao tunataka kujikomboa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *APRM* kama alivyosema mwenzangu aliyetangulia ni kama kioo ambacho tunajihakiki sisi wenyewe kwanza kabla ya kutaka wenzetu ndani ya Afrika waje kutuhakiki. Kwa hiyo unajiangalia wapi hujanawa vizuri, nywele hujachana wapi, umesahau kufunga kifungo kimekatika ili sasa hata wenzio wa nchi nyingine wanapokuja wanakukuta umekaa *smart*. Kwa hiyo na suala hili linatakiwa liangaliwe kwa makini sana. Serikali iwe wazi na kila mmoja ashiriki kwa njia ambayo ataona anachangia maendeleo ya nchi hii. Kila mmoja ni mbia kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana hii nafasi ambayo nchi zinaingia kwa hiari kujipima. Kwa vile hatuna muda huo, kwa kweli sasa hivi tuzibanebane zile nchi ambazo hazijajisajili kwenye hiyo *APRM,* basi nao waingie kwenye utaratibu huu ili Bara la Afrika liondokane na haya magomvi madogo madogo.

Sasa hivi kila wakati kuna ugomvi, tunagombania, tunawapa nafasi maadui kuja hata kupora mali za Afrika. Sasa kama wenyewe tutakuwa makini, ugomvi kama wa Darfur ambayo kwa kweli hayamsaidii mtu yeyote, ni aibu katika karne hii eti bado kuna watu wanataka wakatawale wenzao. Bado kuna watu wanataka kuwa mabwana wengine wabaki kuwa watwana. Sisi tunasema nafasi hiyo haipo, Waafrika wote ni binadamu, sote ni sawa na sote tunataka maendeleo. Kwa hiyo hili suala la kuridhia Mkataba huu nakuombeni wenzangu wote Waheshimiwa Wabunge, kwa bidii sana tuuridhie ili tuweze kufanya kazi muhimu ya kuleta maendeleo katika nchi yetu na bara letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, napenda kutoa ushauri kuwa umefika wakati muafaka vyombo vyetu vya Afrika, Benki na Taasisi nyingine za fedha, ziwe ndiyo vyombo ambavyo nchi nyingi zitajitolea kuwekeza. Hili suala la mali ziko Tanzania lakini Benki iko Ulaya na mali yote inatoka Tanzania inakwenda zake Ulaya au Marekani, tuondoe. Mali iwekezwe hapa Tanzania ikiwezekana ibakie hapa hapa Afrika.

Lakini vile vile Waafrika tuwe na Utamaduni wa kuanza kuaminiana. Wataalamu wetu tuwaamini na tuwatumie. Mimi huwa sifurahii hata kidogo kila wakati inapotokea masuala ya ushauri wa kitaalamu tunakimbilia watu kutoka nje ya Afrika. Lazima tuwape kipaumbele Waafrika wetu katika nchi zetu, Waafrika kutoka nchi za jirani au Taasisi nyingine yoyote na wao ndio dhamana *responsible* kwa ajili ya maendeleo yetu. Kama wanahitaji teknolojia yoyote ambayo labda haiko katika Bara hili, basi wao ndio watatafuta huyo mbia, lakini ile *responsibility* kwa ajili ya mradi ule, inabakia kwa yule mwananchi mzalendo na hasa Waafrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa vile mengi mazuri yamesemwa na tungependa Kuridhia Mkataba huu haraka haraka, basi naomba niseme na mimi naunga mkono na naomba wenzangu wote tuunge mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ABDULLATIF H. ESMAIL:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda kuchukua fursa hii kuwapa Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wote kheri ya mwaka mpya. Vile vile kwa niaba ya Jimbo langu la Mji Mkongwe Zanzibar napenda kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini uliokithiri hauwezi kuondoka bila juhudi. Moja kati ya programu itakayoendeleza chini ya *NEPAD* ni programu ambayo itazingatia kuongezeka kwa ajira na kuinua kipato na uzalishaji mali. Lazima Waafrika au Watanzania kwa ujumla tuwe na njia nyingi za kuzalisha mali kuongeza kipato. Hata Wahenga wanasema, "Sungura mwenye kuishi kwenye shimo moja, hukamatwa haraka." Afrika ya leo inahitaji amani na utulivu, utawala bora unaozingatia demokrasia ambayo vile vile imo katika programu hii ya *APRM*.

Kuna wanafunzi fulani walimwendea Mwalimu wao wakamwambia, tuambie kitu chenye thamani sana. Akawambia ni ushauri. Sasa wakamwuliza, tuambie kitu kisichokuwa na thamani. Akawaambia, vile vile ni ushauri. Wale wanafunzi wakamwambia Mwalimu mbona unatuchanganya? Akawaambia ushauri ukiutumia vizuri utakufaidisha lakini ukiutupa, basi utakula hasara, inakuwa haina thamani kwako wewe. Kwa hivyo *APRM* ni kama ushauri mzuri na hatuna budi kuunga mkono na kuufuata. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa faida ya *APRM* ni kwamba italeta mfumo mzuri ambao utazingatia amani na utulivu, utadhibiti machafuko na migogoro katika nchi zote za Afrika kwa ujumla. Kwa hiyo tutafute njia na kama hakuna njia, basi tutengeneze njia. Kule China Beijing nilikwenda mwaka jana nikaambiwa kwamba "*If you are*

*planning for one year, grow rice; if you are planning for 20 years, grow trees (*miti*) and if you are planning for centuries, grow man*" na hii *APRM* ndiyo inayozingatia manufaa ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Ronald Reagan alivyopigwa risasi kule Washington Hilton mwaka 1981 alipelekwa Hospitali haraka na *group* ya Madaktari akawaambia wakati anapopelekwa chumba cha operesheni huku anacheka, anawaambia; "Nihakikishieni kwamba hamna mpinzani katika nyinyi nyote wa Chama changu." Kwa hivyo inaonyesha kwamba umoja ni kitu kizuri sana. Kuna mshahiri mmoja wa Kifaransa anasema "*Nothing in the world is so powerful as an idea whose time has come*"

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa mchango mzuri kwanza tulioupata kwa Mheshimiwa Njelu Kasaka na Mheshimiwa Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Anne Makinda, Mheshimiwa Remidius Kissassi na Mheshimiwa Abdulatif Esmail. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inatia faraja kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wameunga mkono hoja ya Tanzania kwamba tujiunge na utaratibu wa *APRM*. Labda nigusie pia maneno machache ambayo yamegusiwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni lazima Tanzania na Afrika kwa jumla tuelewe kwamba sasa hivi duniani *fashion* ni nchi kujiunga pamoja ili kujiimarisha kiuchumi na kuwa na masoko makubwa. Ndiyo maana hata nchi za Ulaya sasa hivi kwa maana ya *European Union* bado inaongeza Jumuiya hiyo kuwa na wanachama wengi zaidi ili kuwa na nguvu za kiuchumi. Kwa hiyo hili la *NEPAD* sisi kama nchi za Afrika tukilifuatilia kwa ukaribu zaidi nadhani litakuwa linatupeleka kwenye mwelekeo huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kama Tanzania kuhamasisha nchi nyingine zijiunge na *APRM*. Lakini niliambie Bunge letu Tukufu kwamba katika zile nchi 23 ambazo tayari zimeshajiunga, kwa kweli zinawakilisha asilimia 75 ya idadi ya watu wote wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kwa hiyo ingawaje ni nchi 23 lakini inawakilisha *asilimia ya watu wa Africa* 75. Kwa hiyo kwa kweli tunaendelea vizuri. Tanzania ni lazima tujisifu sisi Watanzania kwa sababu mengi ya malengo ya *NEPAD* tumekwishayatekeleza na tunaendelea kuyatekeleza.

Masuala ya Utawala bora, tunayatekeleza na mengi yao tumeyatungia sheria. Masuala ya kuboresha uchumi wetu tunayatekeleza pamoja na marekebisho mengi katika maeneo mbalimbali pamoja na Serikali za Mitaa. Masuala ya Miundo mbinu tunaendeleza na vile vile miradi ambayo tumeioanisha kwamba ni miradi ya *NEPAD* nina hakika kabisa tumeanza kuifanyia kazi kama Mtwara *Corridor* . Kwa hiyo sisi hatuwezi kuchukua *NEPAD* kama eneo la maegesho ya miradi yetu. Utaratibu huu ni wa hiari kwa sababu nadhani kwa nchi zinazojiunga na *APRM* kwanza zitakuwa zinathibitisha nchi hizo kwamba kweli zinazo uhuru wa Kitaifa ambazo zenyewe inaziamini. Kwa hiyo pana suala la nchi kujiamini.

Lakini vile vile *APRM* kuwa ni ya hiari, maana yake ni kwamba ni kipimo cha nchi kukubali kweli imekubali kuingia katika utaratibu huo. Lakini vile vile nadhani pia ni suala la uungwana. Sio kila kitu, kwa sababu ni nchi za Afrika, basi tusukumane kwa maguvu tu. Mimi nadhani katika maeneo hayo matatu ndiyo maana inafanya *APRM* kujiunga kwa hiari. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kabourou kwamba mara tukishaazimia hili Azimio la *APRM,* Tanzania tutakuwa ndio tunaofuata katika msitari wa kuja kuhakikiwa na huu utaratibu wa *APRM,* kwa sababu hilo ndilo tulilokuwa tunalisubiri. Mimi naelewa sasa hivi hata katika masuala ya utawala bora, uwekezaji kuendeleza uchumi Tanzania tuko katika kiwango cha juu sana katika nchi za Afrika. (*Makofi*)

Mimi nimeshukuru kwa ufafanuzi alioutoa Dr. Makongoro Mahanga kwamba mahusiano na nchi tajiri wametuwekea kama masharti hivi lakini yale masharti ni ya kutuboresha sisi wenyewe. Kuna nchi zingine za Afrika misaada iliyokuwa inapelekwa kule zilikuwa zinafikia mikononi mwa viongozi na zinafunguliwa akiba za fedha nje. Lakini kuna nchi nyingine katika Afrika sasa hivi hakuna mwekezaji yoyote atakayeweza kuwekeza fedha zake pale kwa sababu ya vita.

Lakini vile vile kwa sababu ya kutokuwa na utawala bora katika maeneo mengine, katika nchi zetu za Afrika, hatuwezi kutegemea watu wasaidie maeneo hayo kwa sababu ukiingiza fedha sehemu ambayo ina vita kwa vyovyote haiwezi kuzalisha. Ndiyo maana nasema kwamba ingawa tumewekewa masharti hayo ya utawala bora, uendeshaji, miundombinu, lakini naona ni masharti ya kutuwezesha kuboresha mazingira yetu zaidi, yaani masharti ya uwekezaji.

Nakubaliana na Mheshimiwa Makongoro kwamba kama vile Bunge lilivyohusishwa kwenye masuala ya UKIMWI, idadi ya watu, kwenye suala muhimu kama la *NEPAD* ni vyema tukawa na hoja ya kuanzisha kundi litakalohusika na mambo ya *NEPAD*, kwa sababu hii itasaidia sana katika uhamasishaji. Ni kweli kabisa kwamba lazima tujiulize, kwa nini tumechelewa? Kama alivyosema Mheshimiwa Anne Makinda! Kwa kweli huko nje Tanzania inasifika na nchi nyingine kwamba tunafanya vizuri. Mimi nakubali kwamba yako maeneo mengine ambayo inabidi tuyafagilie, tujiweke sawa na hizo siasa za kuvumiliana. Hapa duniani, hakuna nchi ambayo tunasema eti asilimia mia moja kwa mia moja haina tatizo. Yapo matatizo, lakini nadhani tunafanya vizuri.

Mimi nafikiri *APRM* kama kioo chetu, inatuambia nchi za Afrika tukemee uozo. Tukemee uozo wa rushwa, uzembe, ubadhirifu, uozo wa kutokuwa waaminifu kama alivyosema Mheshimiwa Rais wetu jana kwenye hotuba yake ya mwisho wa mwezi. Ziko nchi nyingine sasa hivi ukitaja sina watu wanasema nchi hiyo bwana hakuna uaminifu. Sisi tunazifahamu. Kuna nchi nyingine ukitaja wanasema, wale matapeli. Sasa nchi kama inapewa sifa ya utapeli huo ni uozo na hatuwezi kuweka uwekezaji katika nchi kama hizo.

Lakini vile vile *APRM* inatufundisha kwamba sasa tumefikia wakati wa kubadilisha fikra zetu na vile vile kuweka mtazamo wetu sahihi kwamba sisi kama viongozi lazima tujue kwamba sasa nchi lazima zijiunge pamoja, watumishi wa Serikali

lazima wajue kwamba nchi zetu za Afrika lazima zijiunge pamoja ili wananchi nao wakubaliane na hayo moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza kwenye Azimio lenyewe, tumesema wadau watashirikishwa wengi tu. Tumesema Serikali yenyewe, Taasisi mbalimbali, *NGOs* na kadhalika. Tumezungumzia pia masuala ya sekta binafsi na nina hakika ushiriki wa Wabunge kwa njia moja ama nyingine utakuwa ni ushiriki ambao ni ule ule unaowawasilisha wananchi kwa ujumla wao.

Kwa hiyo napenda kutoa shukrani za dhati kwa michango iliyotolewa na vile vile nadhani ile *fashion* ya kusema sasa *small is beautiful* kiuchumi inabadilika. Inabidi sasa nchi za Afrika tujiunge pamoja tukuze uchumi wetu, tuibue raslimali zetu ili hii misaada tunayopata kama ya kupunguziwa madeni ije isaidie nguvu tunazoziweka katika kutunza raslimali zetu. Tunahitaji kupunguza upotevu wa mali zetu Afrika, kwa hiyo tuondokane na utaratibu wa kuuza malighafi nje na tuondokane na utaratibu wa kutumia mabenki ya wenzetu kufanyia biashara nje. Kamisheni zinazokwenda ukiziunganisha pamoja ni kiwango kikubwa sana cha pato la Taifa kwa nchi za Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge turidhie *APRM* ili nchi yetu iingie katika mkondo wa kufanya kazi pamoja na nchi za Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimiola Kuridhia Mkataba wa Tanzania Kujiunga na Utaratibu wa Africa Peer Review Mechanism (APRM) lilipitishwa na Bunge)*

*(Saa 12.34 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 2 Februari, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*